

MRADI WA KUANDIKA TAMTHILIA YA "KIZA CHA MCHANA"

NA

MASIIKA DOREEN

2018/KED/1019/F

**MRADI AMBAO UMEW ASILISHW A KATIKA KITIVO CHA ELIMU
KUTOSHELEZA MAHITAJI YA KUHITIMU SHAHADA YA ELIMU YA**

CHUO KIKUU CHA KABALE

MECHI, 2022

UNGAMO

Mimi Masika Doreen nambari ya usajili 2018/KED/1019/F, Ninaungama kuwa kazi hii ni yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa na mtu yejote kwa ajili ya kuhitimu shahada yoyote katika chuo chochote.

.....
16|3|2022.....

MASIKA DOREEN

Tarehe

(M wanafunzi)

IDI-II NI

Kazi hii imekubaliwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kabale.

.....
Tarehe

.....16/3/2022.....

BWANA MULEI MARTIN

(**Msimamizi**)

SHUKRANI

Shukrani za dhati zimwendee Rabana aliyenipa uhai na kuniwezesha kuhitimu kozi yangu. Pia shukrani nyingi zimwendee msimamizi wangu Bwana. Mulei Martin kwa mwongozo wake alioniwezesha kufanikisha kazi hii. Shukrani ziwaendee wahadhiri wote walionifundisha kozi za Kiswahili, sitasahau kutaja majina yenu mionganoni mwao tukiwa na Bwana Agaba Innocent, Bi. Mutenyo Aidah mionganoni mwa wengine. Mungu awabariki kwa kunipa umilisi wa kitaaluma wa Nyanja zote za lugha na Isimu. Maarifa yenu daima itadumu ubongoni mwangu na nitaweza pia kuukuza kutokana na ushauri wenu. Kwa Walimu wangu wa shule za upili na msingi, asante kwa kuniwekea msingi wa kuniwezesha kupata maarifa ya yenu inayonifanya kuitwa msomi na mwalimuwa Kiswahili. Ningependa vilevile niwashukuru wenzangu tuliosoma nao na wale waliochangia katika masomo kwa maarifa na ushauri wao. Mungu awazidishie kwani nimetambua kuwa kidole kimoja hakivunji chawa. Shukrani nyingi ziwaendee wazazi wangu kwa kunilea na kunilipia karo hadi kuhitimu kozi yangu. Mungu awabariki sana. Mwisho, nawashukuru ndugu zangu na marafiki zangu kwa mchango walioitolea kuniwezesha kufikia kiwango hiki cha elimu. Mungu awape Baraka tele.

1.

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia, babangu Bwana Birahuli Eric na mpenzi wangu Bwana Bwarnbale Peter.

MAELEZO YA VIFUPISHO NA MANENO KULINGANA NA MRADI

Ng'onda: Aina ya samaki mdogo sana ambaye ni mkavu.

Kukonda: Kudhoofika; kuwa mwembamba kabisa.

Donoadonoa: Kutiatia uma chakulani bila kukila vilivyo.

Tulipoasi ukapera: Tulipofunga ndoa;tulipooana.

Mori: Ghadhabu ;hasira.

Mavumba: Manoti: Kiasi kikubwa sana cha pesa.

Kujaacheckwa: Kuja pomoni; kujaza kitu mpaka kimwagike.

Kupata nafuu: Kupoa kutoka ugonjwa.

Buheri wa afya: Bila ugonjwa wowote.

Mbilikimo: Mtu mfupi sana; kisheta.

Vipodozi: Malashi yanayotumiwa na wanawake kujipodoa usoni.

Nduma kuwili: Mtu asiyeminika; kigeugeu.

Kiserema: Jembe lililochakaa na kuwa ndogo sana kwa ajili ya kulitumia kwa muda mrefu sana.

Kasri: Jumba kubwa sana.

MUHTASARI WA MRADI

Mradi huu wa tamthilia umepewa anwani ya " kiza cha mchana " kimaksudi. K wa kawaida kiza hujitokeza wakati wa usiku lakini siyo wakati wa mchana kwa hivyo kiza kikijitokeza mchana kuna maana kwamba kuna kitu ambacho hakiko sawa. Mtu yejote azaliwapo huwa anatarajia mema na ufanisi katika maisha yake lakini baadhi ya watu duniani na katika nchi hii, matarajio yao hugeuka ndoto ya mchana yaani huishia yakiwa kinyume kabisa na matarajio ya watu hawa.

Mradi wa tamthilia ya "kiza cha mchana" utadhihirisha wazi wazi jinsi baadhi ya watu wanakumbana na matatizo chungu nzima; tatizo baada yajingine mpaka wanapoanza kujichukia na kulaani siku walizozaliwa. Tamthilia hii itamtia mtu moyo ambaye anakumbana na matatizo katika maisha yake kwamba matatizo ni sehemu ya maisha ya binadamu na sio mwisho wa maisha ya binadamu, wakiyavumilia wakaendelea kujitahidi kadri ya uwezo wao huku wakimwomba Rabana, mwishowe watafanikiwa na hali yao kubadilika kabisa na kuanza kuishi kwa raha mustarehe. Mhusika mkuu, Matatizo ambaye ni fakiri atakumbana na matatizo mengi; moja baada ya jingine licha ya kuwa mchochole wa kupigiwa mfano. Matatizo analemewa na kuanza kujichukia na mwishowe anaokoka na baada ya muda mfupi anafanikiwa na kutajirika kutokana na bahati asiyoilalia wala kuiamkia.

Watu kama hawa huishia kwa kujitia kitanzi baada ya kukumbana na mfululizo wa matatizo kama njia ya kuondokea matatizo haya na kuiacha familia yao katika dhiki kubwa. Kwa hivyo, mradi huu unapinga kabisa kuj itia kitanzi kama suluhisho la mfululizo wa matatizo bali kuwatia moyo na kuendelea kufukuza ndoto zao huku wakiimezea mate machungu hali yoyote ile wanayokumbana nayo mpaka watakapofaulu. Matatizo hapa amechorwa kama maskini, mvumilivu, ili kuwapa watu kama hawa mfano mzuri.

Mradi wa tamthilia utapangwa katika vitendo vitatu na kila kitendo kitakuwa na maonyesho matatu. Kila kitendo kitakuwa na maudhui kuu linalozungumziwa humo ambalo linajitosheleza. Kila onyesho litakuwa na maudhui kuu pamoja na maudhui mengine madogo. Maudhui haya ya vitendo na maonyesho yatachangiana na kukamilishana na kufanya tamthilia nzima yenye wazo kuu la matatizo yaani anwani yenye yewa ya mradi. Maudhui yatakayoshughulikiwa yatakuwa mionganoni mwa utabaka, matatizo, uasherati, migogoro ya kifamilia, uvumilivu, ukengeushi, unafiki, mabadiliko, dini, baraka.

Msanii wa mradi atatumia wahusika mbalimbali ambao ni pamoja na wahusika wakuu, wahusika wadogo, wahusika bapa, wahusika mviringo na wahusika wa kisaikolojia.

Wahusika hawa watakuwa na mienendo ambayo ni pamoja na wavumilivu, wajibikaji, waaminifu, wakengeushi, washerati, wapole, werevu masomoni, washauri wema.

Wahusika wakuu ndio watakaosheheni ujumbe muhimu na wahusika wadogo watawasaidia wahusika wakuu kukamilisha dhamira na maudhui ya msanii. Mazungumzo yataendelezwa mionganii mwa wahusika hawa ambapo nafsi ya kwanza umoja (ni) na wingi (tu) zitatumika hasa kuendeleza mazungumzo baina ya wahusika. Nyimbo, majazi, taswira navyo vitatumika kuwasilisha ujumbe.

Wahusika hawa watakuwa na maleba ambayo yataambatana sambamba na mandhari husika na wazo litakalokuwa likiendelezwa na wahusika hawa. Maleba yatakayotumiwa yatakuwa pamoja na magwanda, majoho ya kitabibu, majoho ya mapadre, ndala, veli.

Maelekezo ya jukwaa yatatumiwa ipasavyo iii kuwaielekeza hadhira kutambua kwa urahisi maleba, miondoko na maingio ya wahusika na sifa zao. Maelekezo ya jukwaa yataandikwa kwa hati za mkazo na kuwekwa katika mabano. Maelekezo ya jukwaa haya pia yataonyesha wakati na mandhari ambapo vitushi vitatendeka. Mandhari haya yatakuwa pamoja na nyumbani, shambani, zahanatini. hospitalini kanisani.

YALIYOMO

UNGAMO	i
IDHINI	ii
SHUKRANI	iii
TABARUKU	iv
MUHTASARI WA MRADI	vi
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI JUU YA MRADI..	1
1. 1. Muhtasari wa sura	1
1.2. Usuli wa mradi	1
1.3. Suala la utafiti	6
1.4. Maswali ya 1nradi	6
1.5. Madhumuni ya 1nradi	7
1.6. Umuhimu wa mradi	7
1. 7. U peo wa 1nradi	7
1.8. Nadharia ya kuandikia mradi	8
SURA YA PILI: MUUNDO NA YALIYOMO KATIKA MRADI.	10
2.1. Utangulizi	10
2.2. Muhtasari wa tamthilia (mtiririko wa hadithi)	10
2.3 Msuko wa kisa katika tamthilia	11
2.4 Wahusika	12
SURA YA TATU: MRADI WATAMTHILIA YA 'KISA CHA MCHANA	14
Onyesho la pili	19
Nyesho la tatu	24
Onyesho la pili	35
Onyesho la tatu	41

KITENDO CHA TATU	46
Onyesho la kwanza	46
Onyesho la Pili:	51
Onyesho la tatu	54

SURA YAKWANZA

UTANGULIZI JUU YA MRADI

1. 1. Muhtasari wa sura.

Katika sura hii, msanii anashughulikia usuli wa mradi, suala la mradi yaam tatizo ambalo linafanyiwa usuluhisho kupitia mradi huu, maswali ya mradi yaani maswali ambayo yatamwongoza msanii wakati wa kutunga mradi wake, madhumuni ya mradi ambayo ni malengo atakayo kutimiza kupitia uandishi wa mradi wake, umuhimu wa mradi, upeo wa mradi yaani mipaka ya mradi na nadharia itakayomwongoza msanii katika kutunga mradi wake wa tamthilia.

1.2. Usuli wa mradi.

Dhana ya tamthilia inafafanuliwa na wataalamu mbali mbali wakitoa maana tofauti tofauti za tamthilia kama inavyooneshwa hapa chini; Mwenda Ntarangwi (2002:169) anaeleza kuwa neno tamthilia limetokana na kitendo "Mithilisha" ambacho maana yake ni kufananisha au kumithilisha hali ya maisha fulani kwa vitendo. Anahitimisha kwa kusema tamthilia ni maigizo ya matukio au visa fulani na uhalisi wake kwa ajili ya kuyasawiri maudhui au maelezo fulani.

Wamitila (2002:7), anaeleza kuwa neno tamthilia kwa upana wake linatumiwa kujulisha
maneno drama na "play" ya Kiingereza. K wa hiyo, tamthilia ni utungo unaoandikwa kwa mtindo wa mazungumzo bora.

Penina Mlama (1983:203) akirejelea na Mulokozi (1996) anasema tamthilia ¹¹¹ sanaa za maonyesho; sanaa ambayo huwasilishwa ana kwa ana tukio fulani kwa hadhira usanii wa kiutendaji. Katika fasili hii, Mlama amezingatia vipengele vya sanaa, uonyeshaji, hadhira, utendaji na tukio.

Sanjari na Mulokozi (1999: 188) wanasema kuwa tamthilia au drama ¹¹¹ fani ya fasihi iliyokusudiwa kutendwa j ukwaani.

Mazrui na Syambo (1992) wanaieleza tamthilia kuwa ni utungo wa fasihi ambaou urnebuniwa kwa kiasi kikubwa kwa lugha ya mazungumzo yenye kuzua na kuendeleza matukio ya hadithi ya utungo huo.

Tuki (2004) nao wanafasili tamthilia kuwa ni utungo wa kisanaa ambao huwasilishwa jukwaani kwa njia ya mazungumzo yanayoambatana na matendo au utendaji ambao husawiri matukio halisi katika jamii husika.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), tamthilia ni kazi ya kidrama na ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira au kazi iliyoadikwa ili kusomwa kimuundo, tamthilia hugawanyika katika matendo na maonyesho, mazungumzo huchukua sehemu kubwa katika uwasilishaji wake wa maudhui.

Kuhusu dhana ya fani, Wamitila (2003) anaeleza kuwa ni dhana inayotumiwa kuelezea muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake.

Mlama (2003) anasema, neno "tamthilia" linatokana kwa maana ya kile ambacho wengi wetu hukiita "michezo ya kuigiza" Tamthilia ni utungo wa drama ambayo ni aina ya maandishi ya sanaa za maonyesho. Anasema, sanaa ya maonyesho ni sanaa ambayo huwasilisha ana kwa ana tukio fulani kwa hadhira kwa kutumia usanii wa kiutendaji.

Kulingana na mwandishi wa mradi huu, tamthilia ni utungo wa sanaa unaoigizwa jukwaani kwakutumia wahusika tofauti ili kufikisha ujumbe kwa hadhira. Uandishi wa tamthilia katika Afrika, Afrika Mashariki na hata Uganda kama nchi umekumbwa na matatizo mbalimbali kama inavyofafanuliwa hapa chini;

Baadhi ya mashirika ya uchapishaji hayako tayari kuchapisha vitabu vya waandishi chipukizi. Jambo hili huwavunja nyoyo waandishi wa Kiswahili ambao wangependa kujiendeleza kitaaluma kuititia uandishi wa vitabu vya riwaya, tamthilia, ushairi, hadithi fupi na fasihi ya watoto. Suala hili ni la kusikitisha kwani imedaiwa kuwa baadhi ya mashirika ya uchapishaji huchapisha majina ya waandishi na wala sio uzito na ufaafu wa kazi yenyewe. Hili hutokea hasa pale mwandishi ametunga kwa mfano riwaya na kisha ikateuliwa kutumiwa Kama kitabu cha fasihi kutahiniwa katika shule za upili.

Mwandishi huyo akiandika kazi yoyote nyingine ya kisanaa, ingawa huenda si ya kiwango cha juu kama ile ya kwanza, kuna uwezekano wa mchapishaji, kuangukia mtego wa kuichapisha kazi ile na kupuuza zile za waandishi chipukizi. Hoja hii inashadidiwa na kilio cha mwandishi wa vitabu vya Kiswahili, Njama (2005) kuwa: Tatizo la kwanza linaanza kwa wachapishaji. Karna

hujajulikana kwenye uwanja wa uandishi, kazi yako haiangaliwi kwa undani sana na mhariri katika shirika la uchapishaji. Miswaada huchukua muda mwangi kutathiminiwa. (Mahojiano kwa njia ya baruapepe)

Ukosefu wa soko ni tatizo lingine linalowakabili waandishi wa vitabu nya Kiswahili. Iwapo mwandishi atachapisha kazi yake na kazi hiyo haina nafasi katika mfumo wa elimu hasa shule za msingi na upili, huenda asipate mauzo mengi. Hili ni kwa sababu mfumo wa elimu nchini Uganda umeibua utamaduni wa kusoma kwa minajili ya kupita mitihani huku dhima nyingine za kusoma zikiwekwa pembedi. Ni kweli kwamba kazi ya uandishi huhitaji kujitolea na kujinyima mengi. Na iwapo juhudzi za waandishi hazizai matunda kwa njia ya kulipwa mrabaha, huvunjwa nyoyo.

Chachage (1993: 25) ameshadidia tatizo la kutegemea soko la shule kuwa: Ni kweli kwamba nchi yetu ina njaa ya vitabu (hasa nya Kiswahili). Hili linakubalika na watu wengi hata wale wanaolalamika kuwa hakuna tabia (utamaduni) wa usomaji. Mashule na vyuo ndiyo masoko yategemewayo na mashirika mengi ya uchapishaji na maduka ya vitabu. Tangu tupate uhuru, mashirika ya uchapishaji na maduka ya vitabu yameshughulika zaidi na vitabu nya mashule na masomo kwa ujumla katika ngazi mbalimbali kama njia pekee na rahisi kuishi.

Uandishi wa vitabu nya Kiswahili mara nyingi huamuliwa na mahitaji ya shule. Wakati mwingine mashirika ya uchapishaji husita kuchapisha kazi ambazo haziwezi kuingizwa katika mfumo wa elimu kama kitabu cha kiada au ziada. Hii ni kwa sababu, soko kubwa la wachapishaji wengi ni shule. Katika mfumo wa elimu nchini Kenya, vitabu ambavyo hununuliwa ili kutumiwa shulenii hasa katika shule za msingi ni vile vilivyoidhinishwa na kuptishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuptitia Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE). Ingawa kitabu cha kiada au za ziada kinawenza kuwa mwafaka, mradhi hakipo katika kijitabu kinachotolewa na Wizara kii twacho "Orange Book". hakiwezi kununuliwa na shule za umma huku ikizingatiwa shule hizi ndizo zenye idadi kubwa ya wanafunzi.

Miswaada ya Kiswahili haitiliwi maanani sana na wachapishaji kwani wanaona kama haina soko. Ni kweli kuwa kila mchapishaji ni mfanyibiashara na kawaada ya kila mfanyibiashara sharti awe na dhamira ya kupata faida kwa kutumia raslimali chache iwezekanavyo. Sekta ya uchapishaji ikiwa ni sekta ya uwezekaji, inafanya kuwa vigumu kwa mchapishaj i kuwekezakatika miradi

anayodhani haitamletea faida. Wachapishaji wengi nchini Kenya hufikiri kwamba soko la Kiswahili si pana kama lile la Kiingereza. Hali hii inaeleza kuwepo kwa vitabu vingi nya fasihi ya watoto kwa lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili.

Kuna waandishi wengi wa vitabu nya Kiingereza nchini Kenya kuliko wale wa Kiswahili. Kwa mfano, orodha ya vitabu nya ziada nya Kiingereza vilivyoidhinishwa kutumiwa katika shule za msingi katika darasa la kwanza mwaka wa 2005 ni 101 ilhali nya Kiswahili ni 19 pekee. Vitabu nya ziada nya Kiingereza vilivyopitishwa kutumiwa katika shule za msingi kutoka darasa la kwanza hadi la nane mwaka wa 2005 ni 659 huku nya Kiswahili vikiwa ni 27 pekee (MoE, 2005).

Mara nydingi waandishi hawapati ushauri ufaao kuhusu taaluma ya uandishi na masuala yanahohusiana na uchapishaji. Akitoa mfano jinsi kazi yake ilivyokawia kuchapishwa kwa sababu ya kukosa ushauri, Mung'ong' o (1993: 49) anatusimulia: Kazi yangu ya awali kabisa ilikuwa Mirathi ya Hatari. Kazi hii ilianza kuandikwa mapema mwaka wa 1966 nilipokuwa katika kidato cha pili katika Shule ya Sekondari ya Kibana. Lakini kwa sababu ya mzigo wa masomo na kwamba wakati ule sikuwa na mtu wa kunishauri katika masuala hayo ya utunzi sikuweza kuikamilisha kazi hiyo hadi mwakal 969. Muswada haukuweza kutoka kama kitabu hadi mwaka wa 1979.

Baadhi ya wachapishaji huwatapeli waandishi, hivi kwamba hawalipi mrabaha kwa waandishi ipasavyo. Wengi wa waandishi wamedai kuwa asilimia 10 wanayolipwa kama mrabaha ni kiwango cha chini mno. Na ni kweli asemavyo Robert (1966: 82) kwamba 'Mwandishi si mtu wa ajabu awezaye kuishi kwa kula hewa na kunywa ukungu. Ni mtu wa desturi ambaye, karna watu wengine wa desturi hafarijiwi na hasara'. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa shughuli ya uchapishaji ni shughuli ngumu yenyeye gharama kubwa kutoka kupokelewa kwa mswaada hadi kitabu kinapomfikia msomaji. Ili kuelewa barabara matatizo yanayowakumba waandishi, tusome dondo lifuatalo:

Popote pale duniani mwandishi wa kitabu anapoketi chini kuandika anategemea vitu vitatu. Kwanza, kitabu chake kitoke vizuri na haraka iwezekanavyo; pili, kisomwe na watu wengi iwezekanavyo; na tatu, apate chochote kutokana na jasho lake. Hivi vikikosekana lazima mwandishi ye yole yule alalamike. (Mall ya, 1993: 24).

Kutokana na nukuu hili matatizo yanayowakumba waandishi yanaweza kuelewa kama ¹¹¹ ya kibinafsi, udhaifu wa wachapishaji na kufujwa na baadhi ya wachapishaji. Jambo hili limewapelekea baadhi ya waandishi kuanzisha kampuni zao za uchapishaji, ambazo nyingi huchapisha kazi za mwandishi huyo mmoja. Ingawa hii ni hatua muhimu ya kukabiliana na baadhi ya matatizo yanawakumba waandishi, mara nyingi kampuni kama hizo hukumbwa na matatizo ya uuzaji na usambazaji wa vitabu hadi kwa wasomaji. Hivyo basi kitabu cha mwandishi kinaweza kutoka wakati ufaao lakini kikakosa kusomwa na kusambazwa kwa watu wengi iwezekanavyo. Kutokana na kutowafikia wasomaji wengi bila shaka, mwandishi hupata mapato machache mno kifedha na hili humvunja moyo sana.

Aidha, waandishi hulalamika kuwa hawapati malipo ya mrabaha na kwa wakati uliokubalika. Isitoshe, baadhi ya wachapishaji hawatoi taarifa muhimu kuhusu kitabu cha mwandishi. Taarifa hii ni muhimu kwani sharti kiwe na maelezo kuhusu kitabu kilitoka lini, idadi ya nakala zilizochapwa pamoja na mauzo ya kipindi fulani, mara nyingi kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Tatizo lingine ni lile linalohusishwa na muda ambaao muswada huchukua ili utathminiwe na uamuzi kufikiwa. Waandishi wengi hulalamika kuwa muda mrefu hutumika katika kupokelewa kwa muswada hadi kutathminiwa na ripoti kutolewa. Na ni kweli mwandishi huweza kungojea hadi mwaka mmoja au zaidi kabla ya kupokea ripoti ya mchapishaji. Lakini mara nyingi wachapishaji sio wa kulaumiwa katika jambo hili. Kwa kawaida wachapishaji huwapa wasomaji wa mswada kusoma na kutathmini mswada hasa ukiwa na kitaalamu. Wasomaji hawa huchukua muda mrefu kusoma na kutoa tathmini ya mswada. Udhaifu mkubwa wa wasomaji ni kuwa wengi ni wenye kazi nyingi hasa za kufundisha katika vyuo vikuu, kufanya utafiti, kuhudhuria kongamano, kuandika miswada, lakini linalomkatisha tamaa zaidi sio muda mrefu ambaao ripoti huchukua kumfikia. La mno ni kuwa ripoti mara nyingi huwa na marekebisho mengi au hukataa muswada mara moja. Mall ya (1993: 215) anasema: Hakuna kinachoudhi mwandishi kama kurudia tena kazi ambayo alifikiri alikwisha kuimaliza mwaka mmoja uliopita. Kinachokatisha tamaa zaidii ni kule kukataliwa kwa mswada na hivyo nguvu za mtu kupotea bure. Lakini ningependa kutoa maoni yangu kuwa ni afadhali ripoti ichukue muda mrefu lakini iwe kamilifu na inayotosheleza. Mara nyingi wachapishaji huwapa wasomaji wa miswada wawili kusoma na kutathmini mswada mmoja. Wakati mwingi jina la mwandishi wa mswada huondolewa kwenye mswada iii kuepuka uwezekano wa upendeleo.

Wakati unavyosonge ndivyo tamthilia ya Kiswahili imezidi kukua na kupanuka na kukuza mbinu za uigizaji. Uigizaji katika tamthilia ya Kiswahili umesambaa na kuvunja mipaka kutoka uigizaji wa maandishi ya kitamthilia hadi kukumbatia uigiziji wa mashairi, ngoma na riwaya.

Teknolojia ya mawasiliano lmekuwakwa hatua kubwa tangu enzi za fasihi simulizi. Katika Afrika, utangulizi wa fasili andishi na mwanzo wa tamthilia nchini Kenya ni mnamo mwaka 1950. Tamthilia ya Kiswahili imejitafutia nafasi yake katika uigizaji wa njia za kisasa kama vile, runinga, redio na magazeti.

Hatahivyo,tamthiliayaKiswahiliilikumbwanavyeanamataifayaKenyanatanzaniakatikaAfrikamas hariki.SerayalughanchiniUgandanamtazamowaKiswahiliulikuwachangamotohalikwambahadileojitihadazakukuzalughayaKiswahilinchinihumozimekuwanachangamotokubwa.

Hatahivyo,nchini Uganda, Mwaka 1960, Serikaliya Uganda iliruhusumatumiziyaKiswahil inchini na kwasasa tuna waandishi wetu watamthilia kama vile Kahaika Masereka Levi" mkwamo"(2018),Innocent Agume "chemachajiwa" ,miongoni mwawengine.

1.3. Suala la utafiti.

Tafiti nyingi zilizofanywa zinahusu vipengele vya tamthilia kama vile maudhui, matumizi ya lugha, wahusika na mandhari katika fasihi. Katika tafiti hizo, watafiti hawajaonyesha mifumo jamii inayojitokeza kutohana na vipengele hivi. Utafiti umezama na kuitathmini mifumo hiyo kupitia kwa tamthilia teule za Kiswahili ambazo ni: tamthilia ya Pango (2003) iliyoandikwa na Wamitila, Kifo Kisimani (2008) iliyoandikwa na Kithaka wa Mberia na Msitahiki Meya (2009) iliyoandikwa na Timothy Arege. Mifumo iliyotafitiwa katika utafiti huu ni: mifumo ya utawala na siasa, utawala katika jamii, utamaduni, imani na dini, utabaka za jamii na elimu ya jamii. K wa hivyo mradi huu wa tamthilia utajikita na kudhihirisha wazi mifumo ya uchumi, elimu. imani na dini jinsi inavyojitokeza katika jamii ya msanii.

1.4. Maswali ya mradi.

2. Ni kwa njia ipi ambayo ninaweza kudhihirisha umilisi wa ujifunzaji wa fasihi ya Kiswahili?
- 3.Ninawezaje kuchangia idadi ya tamthilia za Kiswahili ambazo zimeandikwa katika mazingira ya Uganda kwa ajili ya kukuza na kuendeleza ujifunzaji, ufundishaji au usomaji wa kazi za fasihi ya Kiswahili Uganda?

3. Ninawezaje kudhihirisha masuala ya kimaisha ya binadamu katika mazingira yake, changamoto, na ukombozi wake wa kujenga maisha bora?

1.5. Madhumuni ya mradi.

1. Kudhihirisha ubunifu wa kazi za fasihi unaotokana na umilisi wa ujifunzaji wa fasihi bunilizi ya Kiswahili

2. Kuchangia idadi ya Tamthilia za Kiswahili ambazo zimeandikwa katika mazingira ya Uganda kwa ajili ya kukuza na kuendeleza ujifunzaji, ufundishaji na usomaji wa kazi za fasihi ya Kiswahili Uganda

3. Kueleza maswala ya kimaisha ya binadamu katika mazingira yake, changamoto na ukombozi wake wa kujenga maisha bora

1.6. Umuhimu wa mradi

Mradi huu ukishakamilika, utakuwa na manufaa yafuatayo;

1. Mradi utadhihirisha ubunifu wa kazi za fasihi unaotokana na umilisi wa ujifunzaji wa fasihi bunilizi ya Kiswahili.

2. Mradi utachangia idadi ya Tamthilia za Kiswahili ambazo zimeandikwa katika mazingira ya Uganda kwa ajili ya kukuza na kuendeleza ujifunzaji, ufundishaji na usomaji wa kazi za fasihi ya Kiswahili Uganda.

3. Mradi utaeleza maswala ya kimaisha ya binadamu katika mazingira yake, changamoto na ukombozi wake wa kujenga maisha bora

1. 7. Upeo wa mradi.

Mradi huu hushughulikia masuala ambayo yanayojitokeza nchini mwa msanii. Mandhari yatakayotumiwa ni ya nyumbani, zahanatini, hospitalini, shambani na kanisani.

Kimaudhui, mradi utashughulikia maudhui ya kijamii na kiuchumi. Wahusika watakaotumiwa ni wahusika wakuu, wahusika wadogo, wahusika bapa, wahusika mviringo na wahusika wa kisaikolojia. Hawa watatumwiwa kuwasilisha dhamira na maadili ya kuelimisha, kuonya na kuhimiza hadhira ya msanii.

Mradi unashughulikia kisa cha mwanadamu kukumbwa na matatizo chungu nzima. Msanii anaamini kwamba matatizo ni sehemu ya maisha na hivyo si mwisho wa maisha ya binadamu. Lugha ya mazungumzo itatumika kuendeleza msuko wa vitushi na nafsi ya kwanza umoja na wingi zitatumika kuendeleza mazungumzo baina ya wahusika.

1.8. Nadharia ya kuandikia mradi.

Nadharia inayomwongoza msanii katika kutunga mradi wa tamthilia ya kiza cha mchana ¹¹¹ nadharia ya uhalisia.

Simiyu (2013) anaeleza dhana ya uhalisia kuwa ni tapo au mkabala wa kifasihi ambao husisitiza usawiri wa mambo halisi katika fasihi kulingana na muktadha pamoja na historia ya jamii husika. Mkabala huu umeibua nadharia ya uhalisia ambayo husisitiza kuwa licha ya kazi ya fasihi kunaswa na kutumia ubunifu, kazi hizi husawiri mambo halisi yanayotokea katika jamii husika.

Uhalisia ndio nadharia muhimu zaidi kutokea katika karne ya kumi na tisa na ishirini. Kati kati ya karne ya kumi na tisa huko Ulaya, nguvu za mapinduzi ya kisiasa zilikuwa zikianza kulegea. Mapinduzi ya kiviwanda nayo yalikuwa yamefikia kilele chake. Ulaya ulikuwa umeendelea sana kwa upande wa teknolojia. Wanajamii walianza kukabiliana na matatizo yanayohusiana na miji inayopanuka haraka haraka. Tabaka la makabwela lilizuka. Uyakinifu wa hali ya kibinadamu ulithaminiwa sana. Huu ndio wakati ambapo Karlmax alianza kuzungumzia jamii kisayansi huku akiagua ya kwamba mapinduzi ya makabwela yangetokea baadaye.

Katika mawanda ya fasihi, uhalisia wa matatizo yaliyokuwa yakiwakabili watu uliwafanya wanasanaa kuuhutumu ulimbwende. Matamanio ya kilimbwende yalikuwa ya kinjozi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu.

Walimbwende walikuwa wakijitungia mambo yasiyoweza kutimia. Waliishi ndotoni.

Kutokea mwaka wa 1800 na kuendelea mbele wahakiki na watanzi walianza kuwadhihaki Walimbwende. Gustav Flaubert mmojawapo wa waanzilishi wa uhalisia alishikilia kwamba, "Mtu hufikiria kwa kichwa chake. hafikiri kwa mayo wake. Kwa ufupi. Flaubert alikuwa akilaani na kukejeli dhana iliyowaongoza Walimbwende katika utungaji wao.

Nadharia ya uhalisia inaongozwa na mihimili ifuatayo;

1. Unazingatia njia ya kisayansi katika kutekeleza jambo. Taz Wafula, RM. na Kimani Njogu Nadharia za uhakiki wa fasihi, Nairobi Jomo Kenyatta Foundation 2007.
2. Unasisitiza upinzani dhidi ya mtazamo wa kinjozi juu ya maisha.
3. Unapingana na ulimbwende.
4. Una mashiko katika hali halisi ya maisha ya watu. Unakaribia wasifu na taswira za watu binafsi.
5. Unaonesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao.
6. Unasisitiza muundo na muwala katika kazi ya fasihi.
7. Unaiona kazi ya sanaa kama zao linalojitosheleza yaani ulimwengu ni yakinifu.
8. Wahusika ni vielelezo vyta wanadamu halisi katika ulimwengu unaofahamika.

Wahusika na wahakiki wengi waliotumia nadharia ya uhalisia waliamini kwamba dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli kama ulivyo. Mhakiki naye alimtathmini mwandishi kwa namna huyo mwandishi alivyojibidiisha kuonyesha ukweli.

Haja kubwa ya kutunga mradi wa tamthilia ni kuonyesha picha ya mazingira ambamo jamii inapatikana, mathalani, kioo kinavyotumika kutoa picha za mwananchi katika jamii ya msanii

SURA YA PILI

MUUNDO NA YALIYOMO KA TIKA MRADI

2.1. Utangulizi

Sura huu inahusu muhtasari wa tamthilia, dhamira ya mradi, maudhui, lugha na mtindo, maadili ya mradi, mbinu, msuko wa kisa katika tamthilia na wahusika pendekezwa.

2.2. Muhtasari wa tamthilia (mtiririko wa hadithi)

Mradi huu wa tamthilia umegawanyika katika vitendo vitatu na kila kitendo kina maonyesho matatu ambamo katika kila onyesho mnajambo kuu linalozungumziwa humo pamoja na masuala mengine madogo. Kitendo cha kwanza kinazungumzia juu ya umaskini. onyesho la kwanza linatendekea nyumbani Katika onyesho hili, mgogoro unazuka kati ya Evas na mumewe kutokana na hali mbaya ya umaskini iliyokita mizizi nyumbani humu. Evas anaanza kumlaumu na kumdhara kwa umaskini na kushindwa kuitunza familia yake kama ipasavyo.

Katika Onyesho la pili, Chebeti, mamake na babake wanakula chamcha lakini Chebeti anaonekana hali ila kudonoadonoa chakula. Wazaziwe wanagundua kuwa joto limemzidi na wanampeleka zahanitini bila hela na baadaye Matatizo anampigia bosi wake, Jim anayemlipia bill ya matibabu na kukubaliana kwamba atarudi kazini afanyie deni hilo. Aidha katika Onyesho la tatu, Chebeti, mamake na babake wamo bustanini hawana chakula cha mchana na wanaarnua kula rnaembe. Sonia anafukuzwa shuleni kwa kutornaliza kulipa karo. Wanamtuma kwa jirani yao Kasuku ili aje wamwuze mbuzi wapate karo. Sonia anakuja na Kasuku na anapoenda malishoni kumleta mbuzi nyumbani anamkuta keshauliwa na kamba.

Kitendo cha pili kina maonyesho matatu. Onyesho la kwanza linanaanza na Matatizo anaamuka asubuhi kwenda kazini kwa bwana Jim anapalakiwa na mibweko ya majibwa. Anaenda na kujunga na Godon na wanaanza kuwakama ng'ombe huku wakipiga gumzo. Godon anarnwambia Matatizo kwamba wanawake hawaaminiki. Anaendelea kurntolea utabiri kwarnba usiku huo mkewe atamleta msherauti nyumbani mwake wazame rnapenzini. Kijakazi anangojea maziwa lakini wapi ndipo anapoamua kuja zizini kujichukulia mwenyewe. Jim anakuja na kuwakuta wawili hawa wakizungumza na kuwatukana na baadaye wanaondoka kwenda malishoni. Katika Onyesho la pili, Wakati wa jioni, Jamada anaingia nyumbani mwa Matatizo na

kumletea kilo mbili za nyama na kumpa pesa. Evas anamwahidi kuwa usiku huo watazama mapenzini. Jamada anarudi nyumbani mwake na kubadilisha nguo na kurudi nyumbani mwa Matatizo wakati wa usiku na kuzama mapenzini na Evas kiasi cha kumfanya apige mayowe ya ajabu na baadaye kukimbia akimwacha katika ziwa la damu na tumbo iliyovimba. Kwa kuonge zea Onyesho la tatu, tunamwona Kasuku, mkewe Irene na mwenyekiti wanamchukua Evas hospitalini mpaka wodi ya wajawazito kwa sababu ya tumbo lililovimba. Madaktari wamo katika maandamano kwa kutolipwa mishahara ya miezi mitatu na hivyo wanakataa kuwahudumia mpaka wanaposhauriwa kuwapa chai. Matatizo anaarifiwa na kuja na pesa na kuwakabidhi madaktari na kumtibu haraka haraka na kurudi nyumbani.

Kitendo cha tatu kina maonyesho matatu Onyesho la kwanza linatokea kanisani ambapotunashuhudia Mtume anaanza kuhubiri injili kuhusu uzinzi na Evas anaanza kutiririkwa machozi na wanaita wa kutubu madhambi yao Evas anajitokeza moja kwa moja na kutubu dhambi zake na kumwomba mumewe amsamehe. Matatizo anasogea mbele na wote wanaombewa na kushauriwa kutoa mbegu na kununua maji ya baraka. Hawa wanasalimu amri na kuondoka. Onyesho la pili linatokea Nyumbani mwa Matatizo, hali inabadilika na sasa wanamwomba Mungu bila mchezo huku akifunga. Wanamwomba, kumwamini na kumsujudu Rabana. Katika Onyesho la tatu ambalo linatendeka shambani. Sonia, mamake na babake wanapanda miche ya mibuni kama njia ya kupiga vita dhidi ya umaskini. Kasuku jirani yao anakuja na wazungu na kumwomba Matatizo iii wampe shilingi milioni mia tano, wamjengee nyumba ya kifahari na kumnunulia gari la kifahari. Wanakubaliana na kutia sahihi kwenye hati na baadaye anapokea ujumbe kuwa hela ziwekwa kwenye akaunti yake na wote wanapiga magoti kumsifu Mungu.

2.3 Msuko wa kisa katika tamthilia

Msuko wa tamthilia ni uwiano na maingiliano ya vitushi katika kazi ya tamthilia. Msuko pengine hujulikana kama ploti ya tamthilia. Katika tamthilia, mvutano na mgogoro hukuzwa baina ya mhusika na mhusika mwingine mhusika na nafsi yake, au mhusika na tabaka fulani. Msuko na mgogoro ni msingi mkubwa wa muundo wa tamthilia na uandishi wa tamthilia. Msuko wa tamthilia huwa na sehemu kadhaa. Katika mradi huu wa tamthilia, kila kitendo kitakuwa na suala kuu litakalozungumziwa lakini kitendo hicho kitagawika kwa maonyesho na kila onyesho pia

litakuwa na suala au masuala yatakayozungumziwa humo na vitendo na maonyesho hayo yote yatawiana na kuchangiana kutoka mwanzo hadi mwishoni mwa tamthilia.

Matatizo na mkewe Evas wamo sebuleni wakila chamcha huku Evas akimlaumu mumewe kwa ufukara uliokithiri nyumbani humu. Mtoto wao mdogo, Chebet hali chakula na anaanza kutapika huku hali ikiendelea kuwa mbaya. Hawana pesa lakini wanamchukua zahanatini anakolazwa kwa wiki nzima. Baada ya kurudi nyumbani naye mtoto mwingine anaingia kutoka shuleni baada ya kutumwa kuja kuchukua salio la karo. Jioni iyo hiyo mbuzi wake anakufa. Baada ya siku mbili, Evas anaugua na kuchukuliwa hospitalini anakolazwa kwa wiki mbili. Baadaye. Evas na mumewe anaokoka na kuwa walokole wa kupigiwa mfano, wanaomba sana huku wakifunga na baada ya miezi sita wanajaliwa wanapopewa mabunda na mabunda ya hela kutokana na ardhi yao kuwa na madini ya dhahabu. Maisha ya familia hii yanabadilika kabisa kwani wanajenga nyumba ya kifahari, wanununa gari, watoto wanaendelea na elimu na wote wanaanza kuishi kwa raha na furaha

2.4 Wahusika

Matatizo: Mumewe Evas

Evas: Mkewe Matatizo

Chebet: Mtoto mdogo wa matatizo

Sonia: Mtoto mkubwa wa matatizo; mwanafunzi wa kidato cha tatu

Kasuku: Jirani yao Matatizo na Evas

Bawabu: Mlinda lango wa Life Care Clinic

Daktari: Daktari wa Life Care Clinic

Nesi Maria: Nesi wa Life Care Clinic

Jim: Tajiri; bwana wake Matatizo

Godon: Mtumishi wa Jim katika kitengo cha wanyama.

Kijakazi: Mtumishi wa kikc katika kitengo cha upishi.

Bawabu2: Mlinda lango wa Divine Mercy hospital

Jamada: Mshezati wake Evas.

Mkunga: Mkunga katika hospitali ya rufaa ya Kabale.

Mtume: Pasta katika kanisa la Mungu Mwema la Miracle Centre.

Waumini: Waumini katika kanisa la Mungu Mwema la Miracle Centre.

Wazungu: Wachimbaji wa madini; wanaompa Matatizo mabunda ya

SURA YA TATU

MRADI WA TAMTHILIA YA KISA CHA MCHANÀ KITENDO CHA KWANZA

Onyesho la kwanza

(Nyumbani mwa Matatizo Ni wakati wa mchana saa saba Evas yuko nje akijaribu kumdekeza Chebet ambaye analia kwa njaa inayomwuma sana kwa kukosa cha kutumbukiza tumboni tangu asubuhi. Chebet anaendelea kulia huku mamake kumkaribi)

EVAS: Nyamaa kisirani wee nisije nikakubomoa mie! Wewe na babako ni sawa. Unalia ukiniuliza chakula, babako ameleta kipi? Etinami niliolewa? Niliwasindikiza tu wanawake wengine.

(Matatizo anachomoka ndani na kujitokeza nje huku kajinyenyeyekeza sana)

MATATIZO: Kuna nini mke wangu mpPENDWA? Nini kilichokupata haswa? Nielezee nawe.

EVAS: Eti wanipenda? Wanipenda vipi ikiwa huwezi kunitunza kama mkeo?

MATATIZO (Akichekacheka) Mke wangu mpPENDWA, una maana gani kuniambia hivi? Si najaribu kadri ya uwezo wangu kukutunza na kuihudumia familia yangu?

EVAS: (Akimkaziajicho) Eti nini? Sasa niambie ikiwa wanitunza kama unavyostahili kunitunza kama mkeo.

MATATIZO: (Kimsahalafu) Ukweli ni kwamba mimi na kutunza kama mke wangu ambaye tumezaana mabinti wawili.

EVAS: Sasa unafikiri wajibu wako kama mume huishia kitandani nakunitovifarangawakati wowoteutakao bila kuvitunza vifaranga vyako na kuku wako? Enhe? Au unafikiri kuwa mume ni kuvaal suruali tu. Niambie (*Matatizo anakohoa kidogo kusafisha koo*)

MATATIZO: Mke wangu mpPENDWA, si kama hivyo lakini inakubidi ukumbuke kuwa mtu

hujikuna ajipatapo na tena, la muhimu ni kuishi kwa amani.

EVAS: Basi usingekuwa na uwezo, usingeniletahapa kwako kuanza kutaabika kwahali na mali.

MATATIZO: Sasa niambie ikiwa sikutunzi kulingana na uwezo wa familia yetu. Tena, ni lini nimegombana nawe tangu tulipoasi ukapera?

EVAS: (*Akimkazia macho*) Eti umejaribu kunitunza! Umejaribu vipi hali wakati mwangi twalala tukipiga miayo?

MATA TIZO: Nimejaribusana mke wangu.

EVAS: Umejaribu vipi ikiwa huwezi kuninunulia nguo nzun kama za wanawakewengine ?S inimeshindwa kurudi kanisani kwa maana kilawakat ninapoenda huko, mimi hugeuka mada ya siku na waumini wenzangu.

MATA TIZO: Pole kwa hilo mpenzi wangu. Hata hivyo usijali kanisa sio mavazi ni roho yakoya kumcha Mungu.

EVAS: Unajua ya kuwa watu wamenigeuza wimbo wa kila siku? Siku moja nilitukanwa na muumini mmoja kuwa mimi navaa nguomoja kama mbuzi.

MATATIZO: Usiwajali hao mke wangu mpendwa.

EVAS: Si hayo tu mume wangu. Hebu nikuite mume ... (Mumewe anapandwa na mori na kukunja uso mara moja)

MATATIZO: Sasa niambie. Waniitaje ikiwa huniiti mumeo? Niambie kosa nililofanyakukuto kwenu nikapata jiko nawe?

EVAS: Kosa kubwa la kunitenganisha na hali nzuri niliyokuwemo nyumbani kwetu na kunileta hapa katika hali isiyoweza kuambilika wala kusemezeka.

MATATIZO: Naamini tulikubaliana katika ndoa hii kuishi pamoja kwa hali zote za utajiri na umaskini.

EVAS: Kwa Utajiri na kwa umaskini! Mtu hula utajiri na kuvala umaskini. Wacha hayo, napenda unitunze kama mke wako wa hali zote.

MATATIZO: Nakumbuka nikikutajia wasifu wangu kamili nawe ukani amini ukasema yakwamba pesa sio jambo kuu la kuzingatia katika mapenzi na ndoa, eti la muhimu ni mapenzi ya dhati ...
(Evas anaanzakuchekacheka kicheko cha dharau)

EVAS: Mapenzi ya dhati ni kunisaidia kuondokana na haya hizi kwangu na kwa watoto wako.

MATATIZO: Nimejaribu sana kuwapenda katika hali hii yangu ya uchochole.

EVAS: Napenda nikuelezee kuwa chakula chochote kile hakiwezi kuwa kitamubila chumvi, hali kadhalika, mapenzi hayawezi kuwa na maana ikiwa hayamwagiliwi na mavumba.

MA TA TIZO: Kisichokuwepo mtoto hakililii. (Anatazama juu halafu anaimba)

I wish ningekuwaga na mavumba, Mkwanja manoti, nikuhonge vya thamani. (*Mkewe anaingilia kati*).

EVAS: Hayo ni ya Diamond Platinamu na zake, Najua huna hela lakini inakubidi ujue kwamba mwanamke yoyote yule hawezি kutenganishwa na pesa kama vile ilivyo kwa mbwa na nyama.

MATATIZO: Sasa nifanyeje rnpenzi wangu:

EVAS: Jikakamue, uake mapema, tafuta hapa na pale familia yako ufurahie jasho lako.

MA TA TIZO: Mvumilivu hula rnbivu .Inakubidi ukumbuke ya kuwa hakuna refu lisilokuwna ncha. Siku rnoja kama hii utakuwa mwanarnke wa wanawake. (*Evas anatabasamu kidogo*)

EVAS: Mhuuu! Heri ummke kabla rnajukumu hayajakuzidi. Aliye ma macho haarnbiwi tazamana mwenye nacho hula andazi.

(Chebet anakabidhiwa kipande cha papai lakini anaonekana haonji) Vipi Chebet? Mbona huli?

CHEBET: Mama nataka kunywa chai na kula keki. (Mamake anajaribu kujitia hamnazo lakini Chebet anaendelea kukariri maneno yale yale) Mama nataka kunywa chai na kula keki. Mama nataka kunywa chai na kula keki. (Mamake anamtazarna Chebet halafu anamtazama mumewe kwa jicho la kuulizana)

EVAS: (Akimkabidhi kikombe kilichojaa Chekwa maji) Kunywa maji na kula chakula papai lako. Siyo binti yangu mpandwa?

CHEBET: Mama husikii? Si nimekuambia kuwa nataka kunywa chai na kula keki? (*Evas nad mkewe wamepigwa na bumbuazi. Evas anamgeukia mumewe*) Mtoto huyu ameanza kusema lugha gani? Sisi ambao hatuna msamiati huo katika menu yetu ye ye ameupatapi?

MATA TIZO: Anaweza kuwa amepata hamu na tama ya sijui keki kutoka kwa watoto wenzake hususan walewanaotoka katika aila zenyenye manoti.

EVAS: Huo ni ukweli usiopingika mume wangu. Je, tumfanyieni maskini huyu? Unaona amekataa katakata kula na hata kunywa maji eti ye ye yuataka chai na keki ambavyo hatujui rangi yavyo. Chebet kula papai na kunywa maji yako. Keki na chai tutakupa kesho. Siyo kabinti kangu karembo?

CHEBET: Mama kesho ni mbali mno, siwezi kungojea mpaka muda huo wote mrefu.

EVAS: Sawa basi. Kula tuna kunywa maji yako, jioni nitakupeleknkahawani ukale na kunywa chochote utakacho. Siyo binti yangu mpandwa?

CHEBET: Sawa mama. (Anaanza kula)

EVAS: Umekuwa good girl! Basi kula chakula chako ukakimalize. (Anamgeukia mumewe) Sasa utafanyaje kwani unajua vizuri kuwa binti yako huyu hadanganyiki, ukimwahidi usitimize ahadi huwa shida yenye. Je, una noti yoyote mfukoni mwako tukaona jinsi tutakavyomtuliza?

MATATIZO: Nina elfu moja tu ambazo nimezipangia kununua chumvi kwa maana umeshaniambia kuwa chumvi irneisha. Au siyo mke wangu?

EVAS: Ni ukweli mume wangu. Chumvi ndogo iliyokuwa imesalia niliitia katika Chakulani na ikaisha kabisa na hivyo hatuna ya kutumia kwa chajio.

MATATIZO: (Akimnong'onezea mkewe) Utamranganya tuna kumfanya ayazike hayo katika kaburi la sahau. (Chebet anaanza kukohoakohoa na mara rnoja anamwaga ziwa la mtapiko) Jamani rntoto huyu kapandwa na nini?

EVAS: (Akimpapasa) Chebet! Chebet! Vipi Chebet? (Chebet hajibu lolote ila kukodoakodoa macho kama pan ya aliyanaswa na rntego). Mume wangu mtoto kazidiwa. Joto limepanda mpaka ghorofani. Njooukamweke mkono wako uhisi jinsi alivyoziwa na joto. (*Matatizo akamweka mkono wake na kuchomwa na joto kali utadhani ni lajehanamu*)

MAT ATIZO: Kajitayarische mara moja tumchukue zahanatini bila kukawia kwani hali yake taabani.

EVAS: Sasa utamchukuaje zahanatini ikiwa una shilingi elfu moja tu mfukoni? Kwa nini tusimchukue kwenye hospitali ya umma?

MATATIZO: Hilo ni wazo zuri sana ila tu si kwa nchi yetu arnbayo ufisadi umepanda **mlima Kilimanjaro** hadi kileleni. Mahospitali ya umma hayana rnadawa, madaktari na wauguzi wanagoma kila siku kwa kuwalipwa mishahara duni na hata kurnaliza miezi mingi bila mishahara, wagonjwa wanafia humo kwa wingi sana rnithili ya **SISIIIZI**.

EVAS: Hiyo ndio hali ya nchi tulimo sisi.

MAT ATIZO: Harakisha tu usiulize mengi. La rnuhirnu ni kuokoa maisha, vyta

Malipo vatakuja baadaye. (*Evas anambeba Chebet mgongoni naye*

Matatizo anajiweka tayari) Ushamaliza kijiandaa vilivyo?

EVAS: Naam murne wangu.

(*Wanaondoka*)

Onyesho la pili.

(Zahanatini Ni wakati wa alasiri kama saa tisa hivi, Matatizo na mkewe wamewasili Langoni fa Life Care Clinic huku Evas kambeba Chebet mgongoni naye Chebet anahema mithili ya mgonjwa wa pumu. Bawabu anawaruhusu kuingia zahanatini)

BA WABU: Ingieni tafadhali! (Wanaingia)

Habari zenu ndugu zangu?

MATATIZO: Hakika, habari ni mbaya. Hali ya mtoto huyu taabani kama unavyoona. Si hayati si mamati, tusaidie tu utuelekeze tutakapoelekea moja kwa moja na kupata matibabu ya dharura.

BA WABU: Kwanza jisajilesheni hapa kama ilivyo kawaida yetu hapa kuhifadhi data za msingi za watu wanaoingia humu. Basi mmoja wenu anaweza kuwawakilisha. (Matatizo anaandika kitabuni. Halafu Sawa. Endeleeni moja kwa moja hadi mapokezini mtamkuta nesi ambaye atawasaidia ifaavyo. (Wanaenda moja kwa moja hadi mapokezini wanapokutana Nesi Maria, mwanamke mweusi mithili ya masizi, mrefu kama twiga na tena kakonda kama ngonda utadhani kamaliza miaka na mikaka bila kuramba kwenye chakula au kuonja kinywaji chochote. Anawakaribisha kwa furaha isiyoambilika wala kusemezeka huku uso wake kajaa tabasamu utadhani ni mzazi aliyejifungua salama na baadaye anawakonyeza viti waketi nao wanaketi mara moja.)

NESI MARIA: Karibuni sana ndugu zangu. Basi niwasaidieje?

EVAS: Masaa kama mawili, matatu hivi tulikuwa tunakula chamcha akawa anadonoadonoa chakula tu na baada ya kutumbukiza kitonge kidogo akaanza kumwaga mito ya matapishi, akaanza kukodoakodoa macho huku akihema kupindukia na kupandwa na joto la mwili ndiposa tukajitayarisha na kumleta hapa mara moja.

NESI MARIA: Pole sana mama kwa yote yaliyowafikia lakini mradi ameletwa mapem atapatanaafuu. (Anaandika data kitabuni na baadaye anasimama tavari kuwaelekeza kwa wadi ya watoto)

Mnatoka wapi ndugu zangu?

MATATIZO: Tunakotoka siyo mbali, ni kijijini Mapunda: kijiji chenye punda wa kila aina. NESI

MARJA: Hakika, siyo mbali. Ninyi ni majirani. (Wamefika wodini mwa watoto)

Basi kamlaze mtoto kitandani pale. Naenda kuwaitia daktari na kufumba na kufumbua atakuwa ameishawasili hapa. (Evas Anakabidhiwakitabu chenye data za mgonjwa)
Daktari akija, mpe kitabu hiki. Nawatakieni mema ndugu zangu. (Anaondoka)

EVAS:

Asante mama. (Anamgeukia mumewe) Nesi huyu ni mkarimu sana. Ni mtu mzuri sana, nimevutiwa na uso wake wenyewe tabasamu isiyomtoka utadhani kazaliwa nalo.

MA TA TIZO: Huyu ni mtu mzuri kabisa lakini unalostahili kujua ni kwamba yeyeanafanya biashara na biashara yoyote ile inahitaji ukarimu, la sivyo, biashara hiyo haitafana.

EVAS:

Lakini itakuwaje mume wangu tukipewa bili kubwa ya matibabu hali tumekuja(Daktari, mwanaume mfupi, mkubwa na mweusi kamamakaa anaingia kavaa joho jeupe na miwani. Kim ya halafu)

DAKTARI: Habari zajioni nduzangu?

MATATIZO: Mbaya tu dokta.

DAKTARI: Nakuelewa Bwawa ila tu kwa uwezo wa Maulana, mgonjwa atapataahueni Aminini tu.Basini huyu? (*Akimkonyezea kidole Chebet*)

EVAS: Yuyu huyu doctor.

DAKTARI: Sawa. (*Anafungua kabati anatoa glovu na kuzivaa mara moja.*

*Kimya..... halafu)Basi nikabidhini kitabu chenye data za mgonjwa.
(Evas anamkabidhi kitabu, daktari anapitisha macho haraka halafu anatoa kipima joto na kukiweka kwawani mwa mgonjwa. Kimya. Anawageukia wazazi)Mnajua nini? Mtoto kazidiwa na joto. Ana digrii arobaini sentigredina hizi ni hatari sana kwa mtu ye yote yule na kuna mambo **mengi** yanayosababisha hayo.*

Kwanza anaweza kuwa ana homa ya malaria, homa ya matumbo na mengmne mengi. Sasa nitampima damu ili nipate uhakika wa ugonjwa unaomsurnbua. (*Anatoa sindano na kumshika mgonjwa mkono wa kushoto na kuanza kutafutatafuta mshipa na baadaye anamdunga sindano na kumtoa damu. Nesi Maria anatokea vuu*) Vizuri sana umetokea wakati ulipokuwa unahitajika sana. Kamweke maji mgonjwa huyu, nami naaelekea maabarani, nitarudi muda si mrefu. (Daktari anaondoka na damu naye nesi anavaa glovu mara moja na kuchukua chupa la maji analiweka kwenye mkono wa kushoto wa mgonjwa na kulifanya lining'inie kwenye retort stand na anatoa kichupa cha dawa ya maji, akitumia sindano yake anatoa dawa na kuichanganya na maji. Punde tu maji yanaanza kuteremka kwa kasi kama yamefukuzwa na adui. Daktari naye anaingia na matokeo ya maabara na Kimya kinatawala huku kila mja kamtumbulia macho daktari kwa makini kusikiliza hatima ya maisha ya mgonjwa.)

DAKTARI: Asante sana mwuguzi kufanya hivyo. Aaaa (*Anasita kidogohuku kila mtu katega sikio lake ndi. Daktari anaendelea*)
Nimepima damu ya mgonjwa na matokeo ya maabara ni kuwamgonjwa amezidiwa na homa ya malaria na angecheleweshwa kwa masaa zaidi ya ishirini maisha yake yangekuwa hatarini. (Evas anashtuka na kuonyesha wasi wasi na daktari anamtambua)

Msiwe na shaka kwani mmemleta mapema. Tutafanya lolote liwezekanalo na bila shaka mgonjwa atakuwa buheri wa afya muda si mrefu.
(Maji yamekwisha chupani na mgonjwa kazinduka mara moja na kuanza kuliahuku akimwita mamake)

CHEBET: Mama! mama! Mama nataka chakula.

DAKTARI: Shukrani sana kwa Mwenyezi Mungu. Mradi ameanza kusema na kutaka kula hiyo ni ishara tosha kuwa ameanza kutibika. Hebu tumtie chupa nyininge ya maji. (Akimwambia nesi) Toa chupa hii tupu na

ukaletenyingine pamoja na chloroquine. (*Nesi anasalimu amri ya Daktari anaweka chupa ya maji nyininge iliyochanganywa na chloroquine namgonjwa anatazama mandhari kwa mshtuko na kuanza kuliza mamake*)

CHEBET: Mama tuko wapi? Hawa ni nani? Uuuuiiiii! Uuuuiiiii! (Mamake anamkaribiana kuanza kumbembeleza na baadaye ananyamaa

MATATIZO: Mkewangu mpendwa, hebu njoo tuzungumze kidogo. (*WWanashikanamikono nakwenda nje*)

Unajua nini? Mgonjwa ameanza kuwa vizuri na bila shaka atatudischarge muda si mrefu na unajua kuwa hatuna hela ya matibabu na hivyo ningependa uniruhusu nende kutafuta hela.

EVAS: Utaitafuta wapi mume wangu?

MATATIZO: Usijali mke wangu mpendwa. We niruhusu tu niende nisije nikakawia.

EVAS: Sawa. Lakini niletee andazi na juice nikampe Che bet. (Matatizo anatoka mara moja naye Evas anarudi ndani na muda si mrefu Matatizo anarudi na andazi na juice na kumkabidhi mkewe na anaondoka. Evas anampa Chebet naye Chebet anakula na kunywa kwa hamu na ghamu)

CHEBET: Mama sijashiba. Nataka andazi jingine.

DAKTARI: (Akicheka) Ana hamu kubwa ya chakula na vinywaji na hii ni ishara kuwaamepata nafuu. (Akimgeukia mgonjwa) Unahisije binti yangu mpendwa?

CHEBET: (Akitabasamu) Nahisi njaa kidogo. Nataka kula.

EVAS: Subiri tu baba aje. Atakuletea tu. (Chebet anachecka kidogo)

CHEBET: Ni kweli mama? Nitalila nilimalize na sitakupa. Umesikia mama?
Sitakupaandazi langu. (Matatizo anatokea vuu huku jasho lamtiririka.
Chebet anamwona na kutaka kujiiondoa chupa la maji

kwenda kumlaki kwahamu lakini babake anakuja haraka na
kumzuia)

MATATIZO: Ngoja binti yangu mpendwa. Nimeshakuja mwenyewe, niambie basi.

CHEBET: Baba andazi langu liko wapi? (Matatizo anacheka)
Baba usicheke! Nataka andazi langu.

MATATIZO: Subiri kidogo nitakupeleka mkahawani ule chochote utakacho.

(Chebet anafurahi)

CHEBET: Sawa baba. Nitakula samaki na wali. (Daktari anamchunguza mgonjwa na kukuta
mgonjwa hana taabu yoyote)

DAKTARI: Mgonjwa hana taabu yoyote na hivyo nitawapa vidonge mwende navyo
nyumbani mume mnampa rntoto hadi atakapokuwa buheri wa afya. (Nesi anatayarisha
vibahasha vitano vya vidonge naye daktari anaandika bili ya matibabu ya shilingi elfu
sabini na kumkabidhi Matatizo. Matatizo anarnkabidhi daktari noti mbili za elfu hamsini
naye Daktari anampa Matatizo chenji yake)

Shukrani sana baba! Nawatakieni mema. (Nesi anamkabidhi Evas
vibahasha vya vidonge parnoja na fornu ya matibabu)

NESI: Hapa utampa viwili mara tatu, hapa kimoja mara rnbili, hapa kirnoja mara tatu,
hana kimoja mara mbili na hapa viwili mara mbili.

DAKTARI: Sasa mnaweza kuondoka na kwa taarifa yoyote mtanijulisha kupitia narnbari
yangu hii. (Anarnkabidhi Matatizo kikaratasi chenye nambari yake ya sirnu)

MATATIZO: Asante dokta.

(Wanaondoka)

Nyesho la tatu

(yumbani mwa Matatizo **Ni** wakati wa asubuhi kama saa tano hivi, Matatizo na Evas wameshatoka zahanatini, wanaonekana ni wewe uchovu mwingu.
ote wamekaa bustanini, chini ya mti wa mwembe.)

CHEBET: Kwe! Kwe! Kwe! Baba amepigwa na mwembe (Anaanza kumtikisatikisa) Mama!
Mama we! Baba amepigwa na mwembe. (Matatizo ananyanya kitini na
kuokota mwembe huo)

MATA TIZO: Mradi mwembe huu umenipiga nami sitauhurumia. Nitautumbukiza tumboni
uje kuwa nimekasirika si kidogo. (Anaanza kuungwafura na
baadaye Chebet anaumpokonya mkononi naye anaanza kuuadhibu mara moja)

CHEBET: Baba umekula mwembe wangu. Si unaona urnenibakizia kidogo.

MATATIZO: Una uhakika kuwa mwembe ni wako? Mwembe umenipiga hapa karibu unipasue
kichwa nawe wasema kuwa mwembe ni wako? Chebet usiwe mwongo kiasi
hiki. (Chebet anaanza kumpandapanda babake
mgongoni huku kampaka maji ya mwembe)

CHEBET: Watu wazima hawali maembe baba. Maernbe ni ya watoto kama sisi. U
mesikia baba.

MA TATIZO: Nani kakudanganya huyo kuwa maembe ni ya watoto tu, si ya watu wazima
karna sisi. Si umeona kweli ulidanganywa ukadanganyika?
(Chebet keshamaliza kuadhibu mwernbe na sasa ameanza kumtikisatikisa
baba na baba - mtu kujitia hamnazo lakini Chebet hampi nafasi yoyote ya
kupumuia)
Vipi Chebet wanisumbua kiasi hiki? Huoni kuwa nimechoka kupindukia?

CHEBET: Baba! Baba! Mwernbe si nimemaliza zamani.

MATATIZO: Kwa hiyo? (Chebet anamwambia akiwa kakunja uso wake)

CHEBET: Nataka maembe mengine kwani maembe haya ni matamu sana lakini

kwa maana lilikuwa dogo limenifanya kumeza mate tu.

MATATIZO: Kwa nini usipande wewe mwenyewe? Watu wazima hawapandi miti, watoto kama ninyi ndio wanaoweza kufanya hivyo. Watu wakinikuta mtini itakuwa aibu kubwa kwangu na hata kwa familia nzima. (Chebet anaanza kumpigapiga babake vikali) Unatakani jamani? Ukiendelea kufanya hivi nitakupiga. (Che bet anaanza kulia bila mchezo)

CHEBET: Uuuuiii! Uuuuiii! Embe! Embe! (Babake anasimama na kuokota kijiti na kuanza kuangusha maembe huku Chebet kayaokotaokota)

EVAS: Chebet! Chebet! Ngojea kwanza babako amalize kuangusha maembe yasije yakakupiga kichwani ukaumia. (Chebet anajitia pamba masikioni naye babake anaendelea kuangusha maembe na embe moja karibu limpige Chebet kichwani)
Njoo kaketi hapa Chebet! Kwanza kula maembe uliyokwishakusanya.
(Chebet anasalimu amri ya marnake na anaketi na kuendelea kuadhibu mwembe naye babake anamaliza kuangusha maembe na kuja mara moja na kujikunyata kitini. Wote watatu wanaanza kula maembe)

MATATIZO: Kwa nini usiende ukatayarisha chamcha? Si unaona rnuda wa chamcha unakaribia kuisha? (Anamwambia mkewe naye anacheka)

EVAS: Kwani masaa ya chamcha ni yepi na yasiyo ya chamcha ni yepi? Any way tuache hayo! Wataka nipike nini?

MATATIZO: Si nilileta kilo mbili za unga wa mahindi jana jioni. Usiniambie umesharudi kwa mamake.

EVAS: Kuna kilo moja tu na tukiipika leo kuna maana kuwa hatutapata cha kuweka mekonj jioni na unajua(Sonia, bintio rnkubwa, mwanafunzi wa kidato cha tatu anatokea vuu huku kachoka kwa kutembea safari ndefu na kuchomwa na jua kali na tena kuumwa na njaa na kiu. Wote wanashuka, Kirnya kinajiri kinabaki kukodoleana macho kama mbwa anayemwuguza mwenzake. Sonia anakuja mara moja na

kupiga magoti mbele za wazazi wake na kuwaamkua)

SONIA: Shikamoo baba!

MATATIZO: Marahaba Sonia. Hujambo binti yangu mpewa?

SONIA: Sijambo baba. (Anamgeukia mamake)

Shikamoo mama!

EVAS: Marahaba binti yangu. Kari bu sana nyum bani!

SONIA: Asante mama (Mama anamkagua kwa macho kutoka unyayoni hadi
utosini)

MATATIZO: Imekuwaje ukaja wakati huu? Mmepewa half term?

SONIA: La hasha baba! Walinituma kuja kuchukua salio la karo.

EVAS: Mbona umekonda ukakondeka? Shulen i huli chakula chochote? (Mama
kaduwaa)

SONIA: Tunakula lakini unajua fika kwamba mimi na ugali hatushirikiani. Wiki ijayo
tutafanya mitihani ya kumalizia mwaka na ni sharti ni kwamba kila mwanafunzi
awe amemaliza kulipa ada ya shule.

EVAS: (Anamgeukia mumewe) Sasa tutafanyaje mume wangu? Unadaiwa hela
ulizokopwa ukalipia bili ya matibabu. Hujamlipa Jim na sasa huyu anahitaji
salio la karo. (Anamgeukia Sonia) Unadaiwa kiasi gani?

SONIA: Ni shilingi elfu hamsini tu.

EVAS: Eti elfu hamsini tu! Unajuajinsi ilivyo vigurnu kuzipata?

SONIA: Marna njaa irnenikaba. Hujapika?

EVAS: Nipike nini mwanangu?

MAT A TIZO: Nenda kapike hiyo kilo ya ugali kwani yule bwanangu, Jim alikuwa

kanikopa shilingi laki moja na nimebakiza elfu ishirini kwa hiyo nitanunua cha kupika jioni. Hatuna budi kuuza mbuzi wetu mmoja jioni hii ili tupate hela ya karo. Kwa hivyo nendeni mkamfunge malishoni awe anakula nyasi na mnunuzi ajapo jioni akute ameshashiba atupe hela nyingi. (Sonia anaingia ndani na kuvaan guo za kazi na kumpeleka mbuzi malishoni na kumfunga kwenye nyasi na kurudi nyumbani na kuanza kuandaa chamcha huku wengine wamebaki pale pale wakihisi upemo wa miti ya maembe.)

Unajua nini mke wangu mpendwa? Kesho nitarauka mapema niende mara moja kwa Bwana Jim kuendelea na kazi iii nilipie deni analoniwia. Pesa zitakazotakana na kuuza mbuzi, nilipie salio karo na chenji mtaihifadhi kwa mahitaji ya kila siku kwa mwezi mzima kwani mwezi huu wote sitapewa hata senti moja mpaka mwezi ujao ndio nitakarudia malipo yangu ya mshahara. Unaonaje Mama Sonia?

EVAS: Lakini unajua ya kwamba tuna mbuzi mmoja tuna sasa tukimuza tutakuwa tukifanya maendeleo kweli?

MATATIZO: Naona una wazo zuri ila tu ni kama hatuna hiari yoyote isipokuwa kumuza mbuzi ili Sonia arudi shulen akafanye mitihani yake ya mwisho wa mwaka. Sasa una wazo juu ya njia nyininge ambayo tunaweza kuchangia pesa za karo ya shule?

EVAS: Ikiwa unaweza kupata mtu wa kukukopa hela ungefanya hivyo na ukipewa ujira ungemlipa.

MATA TIZO: Tatizo ni kwamba nitapewa ujira mwishoni mwa mwezi ujao, sasa ni nani atakayengojea kwa muda mrefu kama huo?

EVAS: Nimekuelewa. Hatuna budi kuuza mbuzi. Tutamuza kwani mtu husaidiwa na chakc. (Ni kama saa kumi hivi, Sonia ameshaandika meza na sasa kaja kuwaita kwenda ndani kula)
Sonia vipi? Chakula tayari?

SONIA: Tayari mama. Karibuni mezani kabla hakijapoa. (*ote wanaingia sebuleni kukuta chakula tayari mezani yaani, ugali na kitoweo cha mboga msetowa dodo na nyanya chungu. Chakula cha Matatizo kiko mezani na cha wengine kiko kwenye trei mkekani. anakizunguka na Chebet na babakeweshamega tonge la ugali lakini Sonia anawazuia wasile kabla ya sala.*)

Tafadhali ngojeeni kwanza tukaombee chakula.

Sasa umeanza lini hayo? Hapa si mazoea yetu kuombea chakula. Mbona sasa umeleta msamiati mpya. Sawa basi. Nani atakayeongoza basi.

Mama Sonia unaweza kutuongoza?

EVAS: Sijui mwanzo wala mwisho wake nawe hapa wasema niongoze? Sonia tuongozbasi. (*Sonia anawaongoza kwa salandefu, waanzakumeza mate wakitarajia Sonia kuhitimisha sala yake na wote waseme Amina kwani ndio msamiati tu wanaoujua katika sala lakini Sonia anaendelea mpaka Matatizo anapoilazimu kuhitimisha sala*)

MATATIZO: Amina. (*Wote wanasema Amina ila tu Sonia anayeendalea na sala lakini anakemewa na babake*)

Acha upumbavu Sonia eti ni sala. Wewe unaombea chakula au unasimulia hadithi za mababu? Ni sala gani hiyo inayowafanya watu wameze mate mpaka wanapokosa hamu ya chakula? Unataka tuishiwe na hamu ukile mwenyewe? Basi kula lakini mara nyingine ujaribu kufupisha sala yako. Sawa?

SONIA: Sawa babu. Nisamehe tafadhali!

MATATIZO: Usijali Sonia! (*Wote wanaanza kukiadhibu chakula kwa ukimya kwaniutamaduni wao kutosema mpaka wamalize kula. Chebet amemalizia kula lakinianachukua tonge la ugali na kwenda nalonje. Wote wamemaliza kula na kurudi nje chini ya mti*)

Sonia nenda kamwambie Kasuku aje tumuuze mbuzi. (*Sonia anatii amri*)

Mama Sonia, mi nitaondoka kesho mapema na hivyo nakuomba uwe mwajibikaji, uwatunze watoto, uchunge adabu kama mke wa mtu, hela yoyote nitakayopata nitawatumia kwa simu na ukipata haja yoyote usikawie kunipigia.

- EVAS: Nitafanya hivyo mume wangu mpendwa. (Sonia anaingia na Kasuku, mwanamume mbilikimo, mwenye kinywa kisichokauka maneno)
- KASUKU: Habari gani majirani zangu?
- WOTE: Habari ni hivyo hivyo!
- KASUKU: Mnajua nini? Yule mama, mkewe Kansela ni malaya wa kutupwa kwani janakajakwangu ili nimpe ndizi naye aniruhusu kuingia bwawani nipigembizi mpaka nitakapochoka. (Hakuna anayemjibu) Mnajua binti waTom katungishwa mimba. (Matatizo anamkomesha)
- MATA TIZO: Tuache hayo bwana tushughulikie yalokuleta hapa. Sonia nenda kamlete mbuzi hapa! (Sonia anaondoka)
- KASUKU: Pole sana kwa yallowafika!
- MATATIZO: Tumeshapoa(Sonia anakuja kaweka mikono kichwani na wote wanashuka) Vipi Sonia ukaja bila mbuzi na tena, mikono kichwani?
- SONIA: Mbuzi kauliwa na kamba.
- WOTE: Eti nini? (Hawaajaamini masikio yao)
- SONIA: Mbuzi kauliwa na kamba.

KITENDO CHA PILI

Onyesho la kwanza

(Ni wakati wa asubuhi na mapema, nyumbani mwa Jim, milio ya wanyama inasikika kama vile ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, mionganini mwa wengine. Matatizo anaingia ndani ya geti na kuwakuta watumishi mbalimbali wakishughulika karakara na kazi tofauti tofauti.)

GODON: Karibu ndugu yangu Matatizo!

MATATIZO: Asante kabrother. Habari ya asubuhi na hapa kwa ujumla?

GODON: Habari ni nzuri na hapa ni shwari kama ulivyopaacha. Pole kwa kuuguzza mtoto!
Hali yake sasa?

MATATIZO: Nishapoa na mgonjwa amepoa vilevile.

GODON: (Akiondoka) Nimechelewajamani! Esta anangojea maziwa iii atayarishe stafthi kabla mabosi hawajaamka. Niache niende. Haya baadaye!

MATATIZO: Sawa bwana! Nami naja baada ya kupeleka mzigo wangu na kubadilisha nguo. (Godon *anaelekea zini naye Matatizo anaelekea chumbani mwake*)

GODON: Siina! Siina! (Siina anasimama kwa utulivu huku ndama wake akinyonya maziwa baada ya dakika tatu, nne hivi Godon anamfunza na kuanza kukama huku akiimba)

Hela ni hela j amani,
Hela ni tamu jamani, Tamu
kuzidi asali jamani,
Kanivusha mipaka jamani,
Mke kasahau jamani,
Na watoto jamani,
Hap a nili po j amani,

Ugenini nipo jamani,
Napiga hemajamani, Kama
ni kwangu jamani.

(Matatizo *anaingia na ndoo pamoja na keni na bila kusita anamwendea*
Choozi anamsingasinga mwili na kuanza kumkama)

MATATIZO: Vipi ndugu? Ulikuwa unaongea na nanijamani?

GODON: Sikuwa na mtu yejote bwana.(Anacheka kidogo)

MATATIZO: Basi ikawaje nikasikia sauti tofauti tofauti kama kulikuwa na semina ya walokole? (Godon anamtazama Matatizo na kutabasamu)

GODON: Usinichekeshe nawe kabrother! Si nilikuwa naimba? Unajua nini ndugu?
Nataka nimle saucage yule Kijakazi kwani anaisumbua akili yangu sana.
Akiwa anatembea akidegua matako yake kama hivi (Godon
anasisimama na kuanza kuiga mwendo wa Kijakazi na kabla hajamaliza
Kijakazi anatokea vuu)

KIJAKAZI: Vipi mmechelesha maziwa kiasi hiki? Mwataka kunimwigia unga?
Mabwana zangu wameshaamka, sasa wanatarajia stafthai kuwa
imekwishakuwa tayari kama kawaida. (Kijakazi anamnyakua Godon dumu
mara moja na kwenda nalo)

GODON: Unaonajinsi anavyodengua matako utadhani ni bata mzinga. Huyu
nitammaliza tu. (Anaanza kujiramba midomo)

MATATIZO: Tumechelewa sanajamani. Ngoja tumalizie kazi kwanza tusije
tukajihaini wenyewe.

GODON: Acha uoga nawe! Mwanaume ni mwanaume, huwajabali, si kama wewe mwen
e woga kama wa wanawake.

MATATIZO: Woga ni ngao, wahenga walikwishesema. Sasa si tulikuja kutafuta pesa?

- GODON:** Ingawa tulikuja kutafuta pesa hatustahili kufanya kazi kama punda. Anyway, tuyatupilie mbali hayo. Sasa ningependa unipe mhadhara juu ya jinsi nitakavyofua dafu kula kwenye nanasi yake bila kukawia kwani unajua vizuri kuwa ngoja ngoja kalenga mkia na nangojea kalala kitini. wahenga walikwishesema.
- MATA TIZO:** Sasa sikia unayofikiria. Huna mkeo nyumbani? K wa nini usimwendee ukakata kiu yako badala ya kutiwa nyege na vifaranga usivyojua mbele wala nyuma yavyo. Labda unafikiri kuwa dada yule ni kimada anayejifunulia kila mtu mwenye haja. Si hivyo ndugu yangu. (Godon hajaamini masikio yake)
- GODON:** Eti nini? Umesemaje? (Wanatazamana ... Kimya .. halafu) Brother, unasema hivyo kwa maana hujui mbinu za kumtongoza msichana. Sisi mabingwa katika uwanja huo. Nitatumia mbinu tofauti tofauti nimpe hela yote atakayo (Matatizo amekasirika)
- MATA TIZO:** Eti utampa hela yote atakayo? Kwa nini hela hiyo usiisukumie mkeo ikakidhi mahitaji yake, akajipodoa kwa vipodozi nya kila aina akawa mrembo zaidi ukawa unatiliwa nyege naye mwenyewe badala ya kuishi kwa kunusanusa huku na huku kama mbwa- mwitu. (Godon amechukizwa na maneno ya Matatizo)
- GODON:** Sikia huyu anayonena! We bado unaamini mwanamke? Mwanamke ni nduna kuwili; mkewo ni yule yule unaye kitandani wakati huo. ukiondoka kunakuja wengine anawaita sweetheart, darling, sijui nini.
- MATATIZO:** Hao ni wale makahaba wanaouza miili yao, si mke wa mtu.
(Wamemaliza kukama na wameweka maziwa madumuni. Godon amestaajibishwa na maneno ya Matatizo)
- GODON:** Karibia hapa ndugu yangu nikupigie ramli kuhusu familia yako kwani tulipokuwa tunajibizana nilipokea habari kutoka kwa Mungu na sina budi

kukupasha habari hiyo ingawa ni ya huzuni. Mungu akinipigia kurunzi kuhusu mtu yejote yule nami nikanyamazia taarifa hiyo ni mimi anayeadhibiwa. Basi sikiliza nikwambie.(Matatizo anaingiwa na wasiwasi lakini anajipa moyo na kutega sikio ndi huku kakaa kitako) Mungu amenionesha kuwa unarnwini sana mkeo na ni vizuri kuwa waaminifu lakini sikia haya. (Anasita kidogo huku akimtazama Matatizo usoni ambaye sasa wasiwasi imemzidi) Kabla ya siku hii kuisha utapokea simu kutoka kwa mkeo akikuomba hela ya kukidhi mahitaji ya nyumbani. Wakati huo atakuwa na mwanaume tajiri akimwambia kuwa wewe hukidhi mahitaji yake. Yule mwanaume atamsawishi kwa kumwonesha mabunda ya pesa naye mkeo atakufa kabisa ampe mahaba ya kila rangi na kila umn. Mwanaume huyo atalala na mkeo katika kitanda chako mpaka(Matatizo anapandwa mori)

MATATIZO: Kulala kitandani mwangu?

GODON: Naam! Watamwagiliana mahaba ya kila rangi na ya kila umri mpaka alfajiri mambo yatakavyochacha.

MATATIZO: Kuchacha kivipi ndugu yangu?

GODON: Mwanaume huyo atampiga risasi nyingi kupindukia mpaka mkeo atakapopoteza fahamu na mwanaume huyo akimbie aende zake. Ifikapo asubuhi mwanaume muuza umbea atakwenda kwako abishe mara nyingi bila kufunguliwa. Atawaita watu wauvunje mlango wamkute mkeo taabani wamchukie hospitalini. Ni hayo tu niliyoweza kukufichulia. Mimi napeleka ng'ombe machungani.Niliyokwambia unayajua au siyo?

MATATIZO: Nayajua ndugu yangu. Yule mwanaume muuza umbea anaitwa Kasuku.

Lakini yule tajiri sijamtarnbua, naomba unifafanulie niweze kumtambua.

GODON: Ni mwanaume mfupi hivi, mwenye mvi kichwani, mweusi lakini si mweusi sana na mwenye kigugumizi. Umemtambua?

MAT A TIZO: Nimemtambua anaitwa Jamada. Sasa nifanyeje kuzuia (Jim anatokea mara moja na wote wanakunja mikia yao huku wakitatemeka kama kanga aliyenyeshewa. Godon anashika fimbo yake na kuanza kuwapeleka ng'ombe malishoni naye Matatizo anachukua madumu ya maziwa tayari kuyapeleka nyumbani. Jim anawatazama kwa jicho kali bila kunena kwa dakika mbili, tatu hivi na baadaye anaanza kuwarushia mabomu.)

JIM: Waangalie wapumbavu hawa! Kweli mnafikiri nyie? Sasa ni saa ngapi?
Mlikuja kufanya kazi au mlikuja kueneza umbea wa kijinga hapa?
Pumbavu!

WOTE: Twakuomba utusamehe bwana. Hatutarudia tena. Tafadhali tusamehe!

JIM: Basi kila mtu ashughulikie yake.
(Wanaondoka)

Onyesho la pili

(Nyumbani mwa Matatizo Ni wakati wa magharibi; Evas yuko nje mbele ya jiko kamenya ndizi huku kamaliza mkeka. Chebet yuko upande wa kuume wa mamake mashuka kisu naye anajaribu kumenya ndizi. Mama mtu na huzuni usoni na keshalingia baharini kwa mawazo)

EVAS: Ndizi nimepata lakini sina kitoweo, sasa nitafanyaje? (Anawazaakiwazua)

CHEBET: Mama si unaona najua kumenya ndizi. (Mamake anamtazama kwa hasirana kumkaripia huku akinyakua kisu)

EVAS: Toka! Wataka kujichafua unadhani sabuni tutapatapi hali babako kenda kazini bila kutuachia hata senti moja. (Chebet analia naye mamake anampiga kofi anaanguka chini mara moja)
Unalia? Unalia we pumbavu! Wewe ni mpumbavu kama babako. Eti nami niliolewa? Nililiwa na mbwa eti nilio(Kunatokea mwanaume mfupi,nusu mweusi kavaa suti nyeusi na tai nyekundu shingoni kabeba begi mgongoni. Evas kainama akitia maji sufuriani mwanaume huyu
anamtazama jinsi viambajengo vya nyuma vilivyobanwa na kuanza kumezamate.
Ananyapianyapia nyatunyatu mpaka anapomkaribia na kumgusa matakoni. Evas anashtuka)
Jesus! Umenishtua mayo. Kumbe ni wewe. Karibu sana. (Jamada anajibu kwa kigugumizi chake)

JAMADA: Achante Ebas! Hapari zako na za ha pa?

EV AS: Habari ni hivyo hivyo bwana. Kari bu ndani ! (J amada anacheka kidogo)

JAMADA: Namfuata bwana Matatizo. Yuma ndani au ameenda mjini? (Anajifanya hajui kumbe anajua yote)

EV AS: Matatizo kaondoka juzi na kwenda kazini huko Majani.

JAMADA: (Akiingia) Ok. Sasa unamtarajia kurudi lini?

EVAS: Simtarajii kurudi hivi *karibuni.(Anamwashiria kigoda aketi naye Jamadaanaketimara moja)*

JAMADA: Nilipofika ulikuwa unagombana na nani kwani nilisikia makelele nikadhani labda kumezuka ubishi kati yako na Matatizo. (Jamada anatabasamu huku kamtazama Evas)

EVAS: Usiniambie ya Matatizo! Aliondoka tu bila kutuachia senti yoyote wala kuacha cha kuweka mekon. Leo kama mke nilijaribu kama nilivyoweza nikapata ndizi nikashindwa kupata mboga. Niache rnie! Usinikurnbushe ya Matatizo. Mimi niwiwasindikiza waliolewa.

JAMADA: Usimlaumu murneo mpPENDWA kwani angekuwa na hela, angekuachia lakini chukua simu ukampigie anaweza kukupatia hela kidogo ya kuendesha maisha. (Jamada anatabasamu)

EVAS: Simu haina muda wa maongezi. Nawezaje kushindwa kupata cha kutumbukiza turnboni nikapata muda wa rnaongezi?

JAMADA: Nipe nambari yako nikutumie airtime. (Evas anatafuta nambari yake ya simu katika simu yake na baadaye anampa simu)

EVAS: Ni hii. (Anamkabidhi simu yake. Jamada anamtumia rnuda wa maongezi unaotimia shilingi elfu kumi na baadaye anamrudishia simu ili ampigie mumewe)

JAMADA: Nimekutumia elfu kumi. Unaweza kuwa unatumia hiyo kuongea na watu wako. Ikiisha tutaona cha kufanya baadaye. (Evas ameduwaan na rnara moja anasimama na kumpiga pambaja Jamada lakini Jamada anajifanya kama anataka kumkwepa)

EVAS: Asante sana bwana. Mungu akubariki zaidi. Mbona unanikwepa jamani?

JAMADA: Siyo sanamy dear. Unajua wewe ni mke mrembo wa kupigiwa mfano hapa kijijinina ukweli ni kwamba niliishi kwa kukumezea mate lakini sikupatanafasi ya

kukuambia hayo na kwa hiyo ukinikaribia naweza kupigwa naumeme hali sina wa kunisaidia. (Anasema hayo kupima athari ya maneno yake)

EVAS: Ni kweli nakuvutia? (Anajizungushazungusha mbele ya Jamada)

JAMADA: Chiwezi kukuambia ukaniamini Ebas. Basi mpigie mumeo. (Evas anachukua simu yake anampigia mumewe. Simu inaita kwa muda mrefu na baadaye inapokelewa)

EVAS: Hallo! ee hatujambo. Sasa hatuna chakula, ningependa unitumie hela ya kununua chakula na mahitaji mengine. Eee Huna hela? Tungojee? Mpaka **lini** bila chakula? (Evas anakata simu kabla ya Matatizo kumaliza kumwambia. Matatizo amepiga simu mara mbili lakini Evas anaikata tu)

JAMADA: Anachemaje?

EVAS: Eti hana hela yoyote.

JAMADA: Mume hana pesa ujue hayo lakini usijali mimi nitakusaidia tu kwani unajua mimi nakupenda bila kiasi. (Anafungua begi **lake** na kutoa mabunda matano ya fedha na kuyaweka mezani. Evas viganja kaviweka mdomoni)
Hizi ni nini? Si pesa? Hizi zote unaweza kuzimaliza?

EVAS: Hizi zote ni pesa? (Anaachama mpaka nzi wanapopiga hema kinywani mwake)

JAMADA: Hizi si pesa. Hizi ni kunisaidia tu kukuzukapo haja ya dharula. Nyingi ziko benkini. (Anarudisha mabunda begini na kubaki na bunda moja. Anatoa shilingi laki moja na kumkabidhi Evas. Evas anafurahi sana na kwenda mara moja na kumkumbatia Jamada na kujaribu kumbusu lakini Jamada anaik wepa)

EVAS: Kwa nini unanik wepa jamani? Hutaki busu yangu? Au labda nanuka

kinywa?

JAMADA: Si hivyo Evas. Nina shida moja tu. Ukinibusu tu nitakuwa mgonjwa na najua kuwa hutaki kunitibu nikapona.

EVAS: Nani kakuambia hayo kuwa sitaki kutibu ukapona? Nini nisicho nacho?
Usijali darling. Chochote utakacho mimi nitakupa.

JAMADA: Vizuri basi mahabubu wangu. (Anafungua begi tena na kutoa kilo mbili za nyama ya mbuzi na kumkabidhi Evas)

EVAS: Oooh darling. Asante sana. Wewe ndiwe mume si kama huyu Matatizo eti ni mume wangu. Mume kwa jina tu. Mbwa-mwitu eti ni mume. Wewe usijali tu. Usiondoke naenda kupika, nitarudi nikutolee shukrani ifaavyo.

JAMADA: Hebu niende nyumbani kwanza nibadilishe nguo na kumkabidhi hela hii mke wangu halafu nitamdanganya kuwa nina zamu ya usiku, nije nikute umeshakuwa tayari, mtoto ameshasinzia nikumwagilie mahaba yasiyoambilika wala kusemezeka. Siyo mahabubu?

EVAS: Sawa lakini usikawie kwani mtoto huyu ataanza kusinzia hivi punde.
Haya baadaye! (Evas anamsindikiza Jamada na baada ya kupiga hatua kamakumi hivi, Evas anamkumbatia Jamada naye Jamada anatumia mkono wa kushoto na kuuweka kwenye mlima wa Kilimanjaro naye Evas anaanza kuchekacheka kama mlozi)
Ngojea tu giza litawale ndo utakuja baada ya Chebet kusinzia. Usiogope ukijautakuta mambo yameshaiva upande mlima Kilimanjaro mpaka kileleni(Jamada anaondoka naye Evas anaenda moja kwa moja jikoni na kuendeleana upishi. Ndani, Chebet analia. Mamake kajitia hamnazo. Anaanza kuimba huku kajawa furaha tele)

Mungu u mwema,
Wajua waja wako,
Wakati wowote wawakumbuka,

Masika na kiangazi,
U siku na mchana,
Katika furaha na majonzi,
Nakushukuru sana Bwana, K
wa kuni bariki sana, Mume
tajiri ukanilettea.
Shukrani sana Mungu.

(*Anamaliza kuimba anacheka kicheko cha kichaa na sasa Che bet Kajitokeza nje huku yalia sana utadhani ni nguruwe aliye pigwa mkuki Mamake anamchukua na kumrudisha ndani na kuanza kumbembeleza*) Nyamaa Chebet nikuletee chakula kitamu ukile ukimalize. (Chebet ananyamaa. Mamake anaenda j ikoni anapakua chakula cha ndizizilizosongwa na kitoweo cha nyama ya mbuzi yenyе ladha isiyoambilika wala kusemezeka. Anampa Chebet chakula chake naye anajipakulia chake.

Wanaanza kutikisa masavu kwa hamu na ghamu)

CHEBET: Mama hiki ni kitamu mno. Sijapata kula chakula kitamu kama hiki. Mama umeipatapi nyama tamu kama hii? (*Anangw'afura mnofu na kunywa mafunda matatu ya supu na baada ya dakika mbili anaanza kushikwa na usingizi huku kaweka mnofu kinywani. Evas anamnawisha viganja na midomo na baadaye anampeleka kitandani na punde tu anaanza kukoroma kama chura baharini. Evas anarudi sebuleni anakula haraka na muda si mrefu anaenda bafuni anakoga anajifuta maji kwa kitenge na kujipaka mafuta. Baadaye anajifunga taulo na kwenda kauketi sebuleni kumngojea mgeni wake.*)

EVAS: Karibu ndani! Chebet ameshaingia baharini kwa usingizi kwa hivyo usiogope chochote. Usiku huu ni wetu. (*Jamada anaketi naye Evas ananyanya kwenda kumletea mgeni wake cha kutupa matumbon*)

JAMADA: Unaenda wapi Ebas?

EVAS: Si naenda kukupakulia chakula.

JAMADA: Asante sana babie! Nimeshakula nimeshiba nikashibika. Njoo kaketi hapa nikwambie. (Amemwashiria aketi mapajani naye Evas anasalimu amri maramoja kama askari. Jamada anaanza kumpapasa huku akimwimbia)

Ebas nakupenda, usiniache,
Roho yangu inakupenda, usiniache,
Nakuwaza kila siku, usiniache,
Yote yangu ni yako usinitengete.
*(Ametoa mfukoni noti ya shilingi elfu hamsini na kumkabidhi Evas naye
Evas anapigwa na bumbuazi kitambo. Halafu)*

EVAS: Oooh my God! Hela hii ni yangu yote? (Anaipokea kwa mshangao anaiweka mezani halafu anasimama na kumkumbatia Jamada, wanabusuana huku Jamada kampapasa kwa ustadi wa juu na baada ya dakika kama ishirini hivi,
Evas anaanza kukodoakodoa macho kama panya aliyanaswa na mtego hukukahema kama mgonjwa wa pumu. Taulo inamdondondoka Evas naye Jamada anambeba begani mpaka chumbani mwa kulala na kumbwaga kitandani kama gunia ya viazi)

JAMADA: Mtoto asije akatusikia.

EVAS: Usiogope chochote! Mtoto keshazama baharini mwa usingizi. (Baada ya masaamanne ya mfululizo wa mechili, golikipa Evas, mabao yanamshinda nguvu yakajaa wavuni akaanza kupumua kwa shida lakini Jamada masikio kayatia pamba)
Aiiiiii! Aaaaiiiiiii! Mama weee! Nimekufa mie! (Che bet anazinduka na kuanza kulia)

CHEBET: Mama! Mama! Uuuuuuiiiii! Uuuuiiiii! (*Jamada anaondoka na suruali mkononi*)
(Pazia)

Onyesho la tatu

(Hospitalini Ni wakati wa alfajiri kama saa kumi na moja hivi kwenye lango la hospitali ya rufaa ya Kabale. Kasuku, mkewe; Irene, Chebet na Mwenyekiti wametoka garini huku Kasuku na mkewe wamemshika. Bawabu anawafungulia wanaingia.)

BAWABU: Vipi jamani? Mwafuata nani hapa?

MWENYEKITI: Mama huyu hali yake taabani na hivyo twamtafuta daktari wa kumpa msaada wa dharura kwani(Bawabu anamkata kauli)

BAWABU: Kwani hamna redio?

MWENYEKITI: Redio tunazo bwana.

BAWABU: Basi hamjui kuwa Madaktari na manesi wameandamana kwa sababu ya mishahara duni na kutolipwa marupurupu na mishahara yao kwa miezi mitatu iliyopita? Labda mtafanya hivi; Nendeni kwa private wingi au ikiwa mna chai naweza kuwaitia daktari awasaidie kibinagsi.

MWENYEKITI : Sawa! (*Mwenyekiti anamkabidhi bawabu noti ya shilingi elfu tano*)

BAWABU: Basi nifuateni! Mnaenda kwa wodi ya wajawazito? (Wanamfuata)

IRENE: Naam bwana. (*Anakubali bila uhakika kuhusu wadi wanayostahili kupelekwa Bawabu anawaongoza hadi wadi ya wajawazito na Evas analazwa kitandani halafu bawabu anaondoka kwenda kutafuta mkunga. Mwenyekiti anachukua simu na kumpigia Matatico. Simu inaita kwa muda mrefu na baadaye inapokelewa*)

MWENYEKITI: Hallo Bwana MatatizoHapa hospitalini ya rufaa ya Ka baleMkeo hali yake taabani na madaktari wameandamana kwa hiyo jaribu kuja na bahasha ya kaki. Huna? Bado unadaiwa na bosi wako? Utajaribu?..... Vizuri basi ! Jaribu kuharakisha Unakuja hivi karibuni! Vizuri basi. Asante! (Mwenyekiti anaikata simu)

KASUKU: Anasemaje bwana huyo?

MWENYEKITI: Amesema kuwa bado anadaiwa na bwanake lakini ataenda kujaribu.

Bwana huyu naye ameangukiwa na mikosi maskini wa Mungu.

(Mkunga anaingia, mwanaume mrefu mweusi kavaa joho
jeupe mwenye mapengo kinywani. Anakuja mara
moja kwenye kitanda cha Evas na kumwangalia kitambo halafu ...)

MKUNGA: Mgonjwa ni huyu? (Anawauliza)

IRENE: Naamdkota.

MKUNGA JOHN: Basi lete shilingi laki moja tukamsaidie mara moja.

MWENYEKITI: Bwana hatuna hela yoyote, twakuombeni mtusaidie tu kwani
bwanake (Mkunga amkata kauli)

MKUNGA: Wenzangu mtatusamehe kwani hii ni private arrangement. Mnajua fika
kwamba madaktari na wauguzi nchini nzima wameandamana mpaka
gavumenti itaposikiliza maombi yetu. Msitulaumu, jilaumuni wenyewe
rnlioofanya makosa rnakubwa kwa kubadilisha katiba na kuondoa age and
term limits iii kumruhusu rais Mzee kututawala
kwa kiimla mpaka kifo. Isitoshe, mliendelea na kumpigia kura baada ya
mabaya yote aliyoyafanyia nchi hii. Tunatoka wapi? Tunaenda wapi?
Tazarna umaskini, ukosefu wa ajira, mauaji ya wananchi wenyewe mtazamo wa
mabadiliko, ukosefu wa haki za binadamu, mishahara duni kwa walimu na
madaktari ambao ndio nguzo ya nchi hii huku mawaziri na wabunge arnbao
hawana kazi kubwa ya kufanya nchi hii
isipokuwa kubadilisha katiba, kujiongeza mishahara na kuzuruzuru nchi za
magharibi kila mara, kwenda Kyankwanzi kula nyarna choma huku wakifuja
pesa za mlipa kodi na baadaye wakaingiza nchi kwa rnadeni filiska na kuanza
kumnyonya mwananchi kwa kumuundia kodi za kila aina na tena zisizojali
umri wa mtu kiasi kwamba mtu anaanzia kulipa kodi akiwa turnboni mwa
mamake hadi kufa kwake. Kosa

mlifanya wananchi wenyewe. Mlijisaliti kabisa kwa kubaki kimya huku wakibadilisha katika **iii** wamruhusu Rais Mzee aendelee kutuongoza hadi jehanamu. Mmenielewa? (Hakuna anayemjibu ila kumtazama kwa mshangao tu. Mwanamke mjamzito anaanza kugaragara huku akipiga makelele ya juu sana, wakunga wanamwendea)

MKUNGA JOHN: Vipi mama?

MJAMZITO: Mwanangu nisaidie tu kwani sina hela yoyote. (Matatizo anaingia kabeba begi mgongoni, Mwenyekiti anamkaribia na kumnongoneza sikioni.)

MKUNGA: Mama sina msaada wowote wa kukupa isipokuwa kukuombea kwa M wenyez Mungu ili aweze kukusaidia. Basi mimi naondoka. Anajaribu kuondoka lakini Matatizo anamwona na kumpiga gumi naye Mkunga anatabasamu kidogo)

MKUNGA: Shukrani sana Mzee. Wewe unailewa vizuri nchi hii. (Mkunga anamwendea Evas mara moja.)
Lete kitabu chako.

EVAS: Sina kitabu bwana. (Matatizo anafungua begi na kumkabidhi Mkunga kitabu Mjamzito anagaragara kitandani na baadaye anakata roho)

MKUNGA: Vizuri basi (Anashika kalamu yake mikononi na kuanza kuandika data za mgonjwa)
Basi niambie. Unaitwa nani? Kutoka wapi? Umri wako? Jinsi unavyoumwa na ulipoanza kuumwa?

EVAS: Naitwa Kembabazi Evas, kutoka kijiji cha Rwebishuri, nina umri wa miaka arobaini na minne. Kuumwa na (Anasita kidogo na kugeuka na kukuta kila mtu amtaza huku katega sikio na hamu kubwa ya kujuu balaa iliyomwagika maskini wa Mungu)

MKUNGA: Niambie basi kwani hiyo ndiyo data muhimu ninayohitaji hasa kwa **43**

maana ndio msingi wa matibabu yako. Usiogope wala kufedheheka kwa njia yoyote 11e.

- EVAS: Nasi..... Anasita kidogo na kuwageukia wenzake na kukuta kwamba kila mtu anamkazia jicho. Matatizo amekwisha kasirika si kidogo)
- MATATIZO: Nena tu ugonjwa wako kisirani we au nikuonyeshe kilichomtoa manyoya kanga shingoni. Wacha kutupotezea muda! Pumbavu!
- EVAS: Nanasi nasikia moto chini.
- MKUNGA: Sehemu gani haha?
- EVAS: Sehemu za siri.
- MKUNGA: Ulianenze kuumwa na ulianza lini?
- EVAS: (Akitetemeka) Nilianza usiku mkesha wa leo.
- MKUNGA: (Amekasirika) Serna kinaganaga. Usinipotezee muda mama.
- EVAS: Niliingia uwanjani na mwanaume mwenye bastola kubwa na hata kubwa kupindukia na tena kwa masaa mengi ndipo akanipiga mfululizo wa risasi bila kunihurumia mpaka nilipoanza kuvuja damu nikihisi uchungu mwingi na kufura tumbo kama mnavyoniona. (Kila mtu anaweka viganjamdomoni)
- MKUNGA: Ungefanya hivyo mapema lakini ona unavyotuzungusha. Basi mleteni katika thieta tumhudumie mara moja. Atapona tu mradi amesema wazi. (Kasuku na Matatizo wanamsukuma Evas kwa kijibaiskeli hadi katika thieta. Anapofikishwa humo analazwa kitandani.)
Basi ninyi mnaweza kuondoka na kuita yule mama aliyejuka na mgonjwa huyu kuwa ndiye wa kuja hapa na kumtunza mwanamke mwenzake. (Wanaondoka na mkewe Kasuku anaingia)
- MKUNGA: Kamvue mavazi yote. (Irene anamvua mavazi yote mara moja na

Mkunga bila kusita anamwingiza mgonjwa kipipa kupitia mlima ule na kwa dakika kama kumi hivi maji yote yameshamtoka na baadaye Mkunga anapata kichupa cha oili na kuimimina kwenye glovu zake na kuanza kuimpakapaka kwenye Sehemu za siri kwa dakika kama tano na baadaye anamwacha)
Sasa Unahisije?

- EVAS:** Nasikia vizuri bwana isipokuwa uchungu mdogo ninaosikia kwenye Sehemu za siri. Mungu akubariki sana.
- MKUNGA:** Umeshapona tu! Ule uchungu utapungua pole pole. Kuna dawa itakayokuondoa uchungu mara moja lakini hapa haipo, utaenda uinunue katika maduka ya madawa. (Anamwandikia dawa hiyo kitabuni na Mkunga anaondoka na kuwakuta Matatizo na wenzake wakiwa na wasi wasi mwiningi)
- MATATIZO:** Vipi hali ya mgonjwa?
- MKUNGA:** Amepoa kabisa. Mnaweza kwenda nyumbani kwenu sasa. (Mkunga anainga katika thieta akiandamana na akina Matatizo na kumkuta Evas keshavaa mavazi yake kajawa na furaha tele)
- MATATIZO:** Hali vipi Evas?
- EVAS:** Hali ni nzuri mume wangu. Tunaweza kuondoka. (Evas anavaa viatuvyakenakwenda nje akitembea bila utata na kila mtu ashangaa. Matatizo kwafuraha nyingi anamkabidhi Mkunga noti ya shilingi elfu ishirini.)

- MATATIZO:** Utakunywa chai bwana.
- MKUNGA:** Asante sana bwana. Nawatachia safari njema. (Wanaondoka

KITENDO CHA TATU

Onyesho la kwanza

(*Kanisani Ni wakati wa asubuhi kama saa nne hivi katika kanisa la Mungu Mwema la Miracle Centre. Madhabahu yamepambwa vizuri kwa mapazia ya kijani na mekundu yaliyotundikwa ukutani. Mratibu anaingia na kuchukua kipaza sauti*)

MRATIBU: Masalkheri ndugu zangu katika kristo.

WAUMINI: Masalkheri ndugu.

MRATIBU: Tunakaribia kuanza ibada yetu ya leo na hivyo nakuombeni kwaya kuimba wimbo wa kumkaribisha Mtume na wenzake. Basi simameni nyote tukamkaribishe Baba yetu katika Kristo. (K waya inaimba wimbo na waumini wote wanaimba pamoja)

KWAYA: Washa Washa, Washa moto uwake,

Yesu akija aupate ukiwaka.

(Mtume anaingia kavaa suti ya samawati, shati nyeupe, tai nyeusi na viatu vyeupe pe pe huku kashika Biblia Takatifu na Tablet mkononi. Anaambatana na msaidizi wake pamoja na Mkalimani. Wanaenda moja kwa moja hadi vitini na kuketi. Mratibu anashika kipaza sauti)

MRA TIBU: Shukrani sana wanakwaya kwa kutuongoza vizuri katika wimbo.

Bila kupoteza muda, nitamuita Papa wetu atulishe neno la Bwana.

(Anamgeukia Mtume) Papa you are most welcome. (Mtume anakuja mara moja na kuchukua kipaza sauti na mkalimani wake anachukua kipaza sauti kingine na kusimama upande wa kushoto wa Mtume)

MTUME: Humble your selves before God and we pray. (Wote wanafumba macho yao)

MKALIMANI: Jinyenyekezeni mbele za Mungu tukaombe.

MTUME: *Father in the name of Jesus, we want to thank you for the gift of a new*

day and for your protection up to this great morning. Father we want to commit each and every thing that we are going to say and do be of glorifying your mighty name. In Jesus name we pray. Amen.

I thank everyone who has managed to come to this Sunday's service.

Whoever is here will go back with a lot of blessings.

MKALIMANI: *Namshukuru yeyote aliye weza kuhudhuria ibada ya Jumapili ya leo.*
Yeyote aliye hapa atarudi nyumbani na baraka tele.

MTUME: If you believe what I have said shout Amen.

MKALIMANI: *Ikiwa unaamini niliyosema, paza sauti ukisema Amina. (Wote wanasema Amina kwa sauti yajuu huku nyuso zao zimejaa furaha tele)*

MTUME: *Hebu tusikie neno la Bwana. Mwenye Biblia atusomee Hosea sura ya pili, mshororo wa saba. (Mkalimani anashika Biblia na kuanza kuwasomea)*

MKALIMANI: *"Naye atawafuata wapenzi wake lakini hatawapata; atawatafuta lakini hatawaona; ndipo atakaposema, nitakwenda nikamrudie mume wangu wa kwanza kwa maana hali yangu ya zamani ilikuwa njema kuliko hali yangu ya sasa."(Hosea 2: 7)*

MTUME: *Thank you my brother in Christ. My sister who cheat on your husband, you in danger because that young man you are going with is not loving you at all; he is just after using you and once he uses you, he will start seeing you as a toilet paper before him. God gave you your husband to stay with him in all situations knowing that is the man that suits you but for you you are cheating on him simply because he is poor. My sister this is your time to confess your sins and get saved. God bless you.(Evas Anaanza kutiririkwa na machozi)*

MKALIMANI: Dada yangu unayezini dhidi ya mume wako uko hatarini k wa maana kijana huyo unayetembea naye hakupendi katu. Anatarajia kukutumia tu

na baada ya kukutumia ataanza kukuona kama sashi mbele yake. Maulana alikupa mume wako ili ukae naye katika hali yoyote ile akijua kuwa huyo ndiye mume anayekufaa lakini wewe unazini dhidi yake ya kuwa ni fakiri. Dada yangu huu ndio wakati wako wa kutubu dhambi zako na kuokoka. Mungu akubariki.

MTUME:

For God loved the world so much that He gave his only son, so that everyone who believes in him should not perish but have an everlasting life. (John 3: 16)

MKALIMANI:

Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu sana, hata akamtoa mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.
(Yoh 3: 16)

MTUME:

Any body who wish to confess his or her sins may come forward.

MKALIMANI:

Yeyote anayetaka kutubu dhambi zake anaweza kuja mbele. (Evas anajitokeza mbele mara moja huku akijifuta machozi)

MTUME:

Let's here from our sister. (Mkalimani anamkabidhi kipaza sauti)

EVAS:

(Akilia) Waumini Mungu asifiwe.

WAUMINI:

Asifiwe sana.

EVAS:

(Akijifuta machozi) Namwomba mume wangu anisamehe kwa kumsaliti na kutembea na tajiri mmoja wakati mume wangu alipokuwa nje akitafuta riziki na bwana huyo aliniadhibu vibaya mpaka nikaanza kutokwa na damuna kuvimba tumbo. Nilipelekwa hospitalini na mume wangu mwenyewe akalipa bili ya matibabu. Mume wangu mpendwa unisamehe na Mungu anisamehe kwa kukusaliti na nakuhakikishia kuwa sitarudia tena kosa hilo.

(*Watu wanaonekana wakinong'onezeana*)

MTUME:

Kneel down and you will repeat after me these words; Ooh God I come

*before you as a sinner. I have sinned against you and against my husband.
I ask for pardon of my sins and delete my name in the book of sinners and write it in the
book of holy ones. Amen. (Evas anarudia maneno yale yale na Mtume anamweka
mkono kichwani na kumwombea) Mume wa dada huyu aje hapa tumwombee.
(Matatizo anakuja mara moja na kupiga magoti mbele ya Mtume kwenye upande wa
kuume wa mkewe na Mtume anaanza kuwaombea)*

*Father in the name of Jesus, we call upon you to come and unite this couple and bless
them with whatever they desire; bless them with wealth, children food and peace In
their family so that they will be able to glorify your name. In Jesus name we pray.
Amen.*

*My brother make sure that you sow a seed so that it acts as a foundation
for your blessings.*

MKALIMANI: Kaka yangu hakika upande mbegu itakayokuwa msingi wa baraka
zenu. (Matatizo anatoa noti ya shilingi elfu kumi na kumkabidhi Mtume)

MTUME: Mungu awabariki sana. Mbegu hii mliyopanda itawazalia matunda chungu nzima
kabla ya mwezi huu kuisha.

MATATIZO: Amina.

MTUME: Don't forget to buy blessed water outside cos it is so powerful and full of
blessings.

MKALIMANI: Msisahau kununua maji ya baraka nje kwa maana ni yenye nguvu zaajabu na
yamejaa baraka.

MTUME: Ok let's pray and end our service.

MKALIMANI: Hebu tuombe tukamalize ibada yetu.

MTUME: *Father we thank you for we have managed to reach the end of our service successfully.
Guide everyone to his or her home, bless them and stay with them always.*

WAUMINI: Amina. (Waumini wote wanatoka na nje wanaonekana wakinunua maji ya baraka na Matatizo anawasukuma wenzake mpaka kwa muuza maji)

KIJANA: Maji ya baraka! Maji ya baraka! Maji ya baraka!

MATATIZO: Kichupa unakuza kiasi gani?

KIJAKAZI: Kichupa kidogo ni shilingi elfu kumi, chupa kikubwa ni elfu thelathini, lita tano ni shilingi elfu hamsini na jerikani ya lita ishirini ni shilingi laki moyo.

MATATIZO: Basi nipe kichupa kidogo. (*Anamkabidhi noti ya shilingi elfu kumi naye Kijana anamkabidhi Kichupa cha maji*)

KIJANA: Asante brother.

MATATIZO: Karibu ndugu.
(*Wanaondoka*)

Onyesho la Pili:

(Nyumbani mwa Matatizo Ni wakati wa asubuhi na mapema kama saa kumi na mbili hivi, Evas ameshatoka usingizini na kuwasha karaboi na kuiweka mezani.. ote wanajumuika sebuleni na ambamo mna Biblia na maji ya baraka mezani na daftari na kalamu. Evas anawaongoza kuimb@)

WOTE:

Tutembelee Tutembelee, Malaika
wa Mungu Tutembelee, Kwa
vijana utembelee,
Malaika wa Mungu Tutembelee K
wa waume utembelee, Malaika wa
Mungu Tutembelee K wa
wanawake utembelee, Malaika wa
Mungu Tutembelee.
Wote wanafumba macho yao na Evas anawaongoza katika sala

EVAS:

Babetu uliye mbinguni tunakushukuru sana K
wa ulinzi wako unaotupatia kila siku
Baba, sisi ni maskini wasio na mbele wala nyuma
Lakini Baba wewe ulitupenda ukaja kwetu kututafuta ambako hakukuwa na njia. Baba u
mwema, hakuna yejote anayeweza kulinganishwa nawe.
Baba tunakushukuru kwa tuliyoyapitia
Mabaya na mazuri ulikuwa nasi
Babetu hujapata kusinzia hata chembe
Baba tunakushukuru kwa kutulisha na kutunywesha Sisi
makabwela wako
Wewe ndiwe Mungu asijejali asili wala fasili ya mtu
Unawajali wabaya na wazuri ndio maana ulituokoa
Sisi waovu ukatuosha na damu ya yesu kristo
Baba ndiwe wewe mwenye uwezo wa kubadilisha kila hali ya mtu Baba
tunakuomba uje ubadilishe hali ya familia yetu Wanaotuchekela kwa
ulitima wetu waone fahari yako Bwana.

Kama ulivyokuja kututafuta iii utuoshe madhambi yetu vilevile katujaze nabaraka zako Ewe Bwana, Mungu wa majeshi. Tupe hela ili tuweze kukusujudia bila upungufu wowote Ewe Bwana. Tupe baraka za uzima, amani, upendo, vyakula. Tuondolee iblisi mwenye kutuletea magonjwa na matatizoyanayotudhoofisha katika imani yetu.

Unasema katika Biblia Takatifu, "Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyimtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa. K wa maana kila aombaye hupokea naye atafutaye huona, naye abishaye atafunguliwa. (Matt 7: 7-8) kwa hivyo tumekuomba hayo yote tukiamini kuwa utayasikia maombi yetu. Tumeomba hayo yote kupitia jina mwanao Yesu Kristo.

WOTE: Amina!

EVAS: Shukrani sana nyote kwa kushirikiana nami katika dua za asubuhi.
Siku ya leo, kesho na kesho kutwa ni siku za kufunga kavu yaani hakuna yeyote atakayeranba kwenye chakula, kinywaji au tunda lolote lile mpaka saa kumi na mbili jioni, jua litakakalopunga. Muda wote huo ni kuomba kwa Mwenyezi Mungu, kumsifu na kumwabudu kwa nyimbo na kusoma neno lake katika Biblia Takatifu. Tuko pamoja wenzangu?

MATATIZO: Sawa mke wangu mpPENDWA lakini naomba Chebet awekewe chakula chakekando kwani umri wake haumwezeshi kufunga kavu kwa masaayote hayo bila kuramba kwenye chakula au kinywaji chochote kile.

EVAS: Sawa mume wangu mpPENDWA. Nitampikia Chebet chakula chake tu.

SONIA: Mama na mimi nitakula kwani tulizoea kunywa stافتahi, chamcha na chajio na kwa hivyo siwezi kufika jioni bila kutumbukiza chochote ndani. Nitakufa tu kwa njaa.

EVAS: Sasa niambie, ni siku ngapi tulizoshindwa kupata cha kuweka mekoni na hivyo tukajilazimu kufunga mpaka saa mbili usiku tunapokula chajio?

SONIA: Mama siku hizo tulikuwa hatuna hiari yoyote juu ya kufunga lakini sasa

naona tuna mkungu wa ndizi ndani, sasa nitaumwaje na njaa nikiona ndizi ndani a vifaa vyote vyaa kupikia ndani?

EVAS: Sonia mwanangu, usione kufunga kama adhabu kwako bali ukuone kama njia mojawapo ya kufungua milango yote ya baraka zako. Hebu nikuulize basi. Huna vitu unavyotaka Mungu akupe?

SONIA: Ni vingi mno mama. Kwanza namwomba Mungu anipe karo na akili masomoni, nisome hadi chuo kikuu nihitimu kama mhandisi mjenzi niwajengee nyumba inayopendeza sana na mengine mengi.

EVAS: Basi kama tulivyokwishasikia neno la Mungu katika Matt 7:7- 8, Ombea hayo yote na bila shaka Mwenyezi Mungu atakuja sikia maombi yetu na sisi sote tutafurahi. Basi jitayarisheni kwa maombi ya leo. (*Wanaanza kuimba*) Bwana u mwema,
Bwana u mkubwa,
Ujuu ya hali yoyote,
Umejaa baraka na usamehevu
Bwana nitakusifu daima.

(*Wote wanaondoka na kwenda nje.*)

Onyesho la tatu

(*Shambani Ni wakati wa asubuhi kama saa mbili, tatu hivi shambani mwa mbuni, Matatizo, Evas na Sonia wamevaa magwanda huku wameshika majembe kwa ustadi wa juu wakichimba mashimo ya kupandia mbegu za mbuni ili kujitayarishia siku zao za usoni. Chebet naye kashika kiserema chenye mpini mdogo na tena mfupi yuko nyuma ya mamake anajaribu kumwiga anavyochinba mashimo na kufanya hivyo baadaye*)

MATA TIZO: Mibuni hii tunayopanda itakuwa tayari kwa mavuno miaka mitatu ijayo kwanimiti hii michache iliyo tayari kwa mavuno niliipanda miaka mitatuiliyopita. Mibuni ukiitunza vizuri hukuletea kipato kikubwa na katika miakamichache tu, maisha ya mtu yanaweza kubadilika kabisa. Niliona ni bora nihamishe ujuzi na mbinu zinazotumiwa kwa bosi wangu katika mashamba yake nizitumie kujanzilishia mashamba yangu mwenyewe nami nijipatie kipato niache kuwatumikia mabwana wanaotunyonya kwakutufanyisha kazi kama punda nkujitajirishasha wenyewe kutokana na jasho zetu.

EVAS: Hilo ni wazo zuri mume wangu mpendwa. Rais Mzee anatwambiaga kuwa tujishirikishe katika kazi zinazotuletea kipato kama vile kulima Mibuni.

(Anasita kidogo akijaribu kutoa udongo shimoni) Mibuni ingekuwa mizurilakini tatizo ni kwamba inakawia kwa tayari kwa mavuno.

MATA TIZO: Hilo si tatizo kwani mibuni inakaa nje nawe unataka ndani sasa kungojea tukutakuathiri kivipi?

Hata ukiwa inakawia kuvunwa si unapita yule
aliyekataa kuipanda kuwa inachelewa kuvunwa?

SONIA: Baba unayosema ni ukweli kwani mwalimu alitwambia methali kuwaniherikuchelewa kuliko kutofika hata kamwe na tena, sisi kama wakristo inatulazimu tuwe wavumilivu na mwishowe tutakuja faulu.

EVAS: Sawa basi. Huo ndio umuhimu wa kuelimisha mtoto wako. Si unaona mtoto ameanza kunichallenge.

CHEBET: Mama! Mama! Mama si unaona najua kulima mashimo?

EVAS: Toka nyuma yangu nisije nikakukata kwajembe ukaniangushia baala. (Mamake anamnyakua Chebet kiserema chake na Chebet anaanza kulia)

MATA TIZO: Ikiwa mnachimba mashimo haya, jaribuni kuyarefusha *kidogo chini* na kwa upana ili tupate nafasi ya kuwekea mbolea.

(Kunajitokeza wazungu watatu wakiongozwa na Kasuku na akina Matatizo wanaanza kuingiwa na wasiwasi mwingi huku wakiwakazia macho *wakiwa na hamu kubwa ya kusikia walilokujia* wazungu *hawa*)

KASUKU: Habari *zenu* marafiki zangu?

MATATIZO: Habari ni njema ndugu yangu mpendwa.

KASUKU: Nimewaletea wageni hawa wanapenda kuongea nanyi na kwa hivyo nakuombeni mwasikilize.

KASUKU: Sawa brother. (Kasuku anawageukia wazungu na kuwaashiria waongee naMatatizo)

WAZUNGU: Good morning my dear friends?

MAT A TIZO: Good morning to you all. You are welcome to our place.

WAZUNGU: Thank you my dear. We found out that your land is Rich in gold and we would like to give you five hundred million ugandan shillings, we buildfor you a permanent mansion and buy for you an expensive car. Is thatone okay for you?

MATATIZO: (Akitabasamu) It is okay my dear ones.

W AZUNGU: Then sign this memorandum of understanding and you give us your account number and tomorrow our Engineers will start construction of your mansion and they will come with your car. (Matatizo anatia sahihi yake na kuwapatia nambari ya akaunti yake na wazungu wanaondoka)

EVAS: Walisemaje?

MATATIZO: Mungu amejibu maombi yetu mke wangu mpendwa. Ardhi yetu ina madini ya dhahabu na hivyo watatulipa shilingi milioni mia tano, watujengee kasri na kutuletea gari la fahari kuanzia kesho.

(*Tahadhari ya ujumbe inasikika na Matatizo anaisoma kwa sauti ya juu na tena kwa furaha isiyoambilika wala kusemezeka*)

You have received five hundred million Ugandan shillings on your account. (Ujumbe anaonyesha Sonia naye anausoma na wote wanaanza kuimba)

WOTE:

Mungu u mkubwa,

Wewe hulali katu, U

metukumbuka,

Asante sana B wan a.

(*ote wanakumbatiana wanapiga magoti tayari kumsifu Mola*) (*Pazia*)

Mwisho